

# Mwongozo wa Haki za Mzazi katika Elimu Maalum

## Taarifa ya Ulinzi wa Utaratibu wa Elimu Maalum

Aprili 2017

Ohio | Idara ya Elimu

## Kuhusu Elimu Maalum

Elimu maalum, kwa wanafunzi wa miaka 3 hadi 21, inaongozwa na mahitaji ya serikali na jimbo. Mahitaji ya serikali yanarejelea Sheria ya Elimu kwa Watu walio na Ulemavu (IDEA). Mahitaji ya jimbo yanarejelea Viwango vya Utenda Kazi vya Ohio kwa Elimu ya Watoto walio na Ulemavu (Viwango vya Utenda Kazi vya Ohio).

Mwongozo huu unaweza kukusaidia uelewe haki zako na haki za mtoto wako kulingana na IDEA na Viwango vya Utenda Kazi vya Ohio. Pia unakupa maelezo na raslimali ili kukusaidia uelewe usaidizi na huduma za elimu maalum kwa mtoto wako.

Wilaya ya shule ya eneo lako pia inaweza kukusaidia uelewe haki zako chini ya sheria hii. Ikiwa una maswali kuhusu maelezo yaliyoko kwenye mwongozo huu, tafadhali wasiliana na mkurugenzi wa elimu maalum katika wilaya yako.

## Mtu wa Kuwasiliana Naye katika Shule Yako kuhusu Elimu Maalum

Wilaya: *Tafadhali ongeza maelezo yafuatayo kwenye sehemu hii ya mawasiliano:*

**Mkurugenzi wa Elimu Maalum:**

**Nambari ya simu:**

**Anwani ya barua pepe:**

### Mtu wa Kuwasiliana Naye kuhusu Elimu Maalum katika Idara ya Elimu ya Ohio

(Simu) 614-466-2650

(Simu isiyolipishwa) 877-644-6338

(Faksi) 614-728-1097

25 S. Front Street, Mail Stop 409
Columbus, Ohio 43215

Exceptionalchildren@education.ohio.gov

Kwa wapiga simu wanaotumia printa ya mawasiliano (almaarufu TTY), tafadhali piga simu katika Huduma za Ohio Relay kupitia (800) 750-0750.

Maelezo ya Ziada ya Mawasiliano http://bit.ly/2hgiNa1

## Utangulizi wa Mwongozo huu wa Haki za Mzazi

Sheria ya Elimu kwa Watu walio na Ulemavu (IDEA) inalinda haki za wanafunzi walio na ulemavu na haki za wazazi wao. Mwongozo huu unakueleza kuhusu haki hizo. Shule yako ni lazima ikupe nakala ya mwongozo mara moja kila mwaka ikiwa mtoto wako anapokea huduma za elimu maalum. Wewe pia lazima upokee nakala:

- Ikiwa utaomba mtoto wako afanyiwe tathmini kwa sababu unahisi kuwa mtoto wako anaweza kuwa na ulemavu;
- Ikiwa wilaya ya shule yako inataka mtoto wako afanyiwe tathmini kwa sababu inahisi kuwa mtoto wako anaweza kuwa na ulemavu;
- Ikiwa utatuma (utawasilisha) *lalamiko* – katika maandishi – kwa Ofisi ya Watoto wa Kipekee katika Idara ya Elimu ya Ohio, na liwe lalamiko lako la *kwanza* katika mwaka wa shule;
- Ikiwa utatuma (utawasilisha) ombi – katika maandishi – kwa Ofisi ya Watoto wa Kipekee katika Idara ya Elimu ya Ohio kwa ajili ya *mchakato wa utatuzi* wa mgogoro kuhusiana na elimu ya mtoto wako, na ni mara yako ya kwanza katika mwaka wa shule ambayo umeomba hilo;
- Ikiwa mtoto wako *ameondolewa shuleni kwa sababu za kinidhamu (tabia)* – na mtoto wako tayari ameondolewa kutoka shule kwa siku 10 au zaidi wakati wa mwaka wa sasa wa shule; au
- Wakati *wowote* ***unaomba*** *nakala ya mwongozo.*



## Yaliyomo

**Maelezo ya Jumla** .......... **5**

Idhini ya Mzazi Baada ya Ufahamu
Je, Mtoto Wako Anastahiki Elimu Maalum?
Tathamini Huru za Kielimu
Taarifa ya Mapema ya Maandishi

**Rekodi za Kielimu** .......... **10**

Ufikiaji wa Rekodi

**Utatuzi wa Mgogoro** .......... **12**

Mchakato wa Utatuzi wa Mgogoro
Utatuzi wa Mapema wa Lalamiko
Uwezeshaji
Upatanisho
Kuandikisha Lalamiko la Jimbo
Mchakato wa Ukiukwaji wa Sheria ya Jimbo
Kutuma Lalamiko la Mchakato
Utatuzi wa Mgogoro Mfululizo wa Matukio Katika Mchakato
Utatuzi wa Mgogoro Utatuzi katika Mchakato wa Utatuzi wa Mgogoro
Mchakato wa Usikilizaji
Kukataa Rufaa kuhusu Uamuzi katika Mchakato wa Utatuzi wa Mgogoro
Hali ya Mtoto Wakati wa Mchakato wa Utatuzi wa Mgogoro
Ada za Mwanasheria

**Nidhamu** .......... **29**

Taratibu za Adhabu kwa Watoto walio na Ulemavu Kubainisha ikiwa
Kosa Lilitokana na Ulemavu
Mpango Mbadala wa Kushiriki Elimu ya Kawaida

**Uwekaji katika Shule Binafsi wa Watoto walio na Ulemavu na Wazazi kwenye Shule Binafsi kwa Gharama za Umma** .......... **32**

Mchakato wa Kubaini Kurejesha Gharama

**Taarifa kwa Mzazi kuhusu Mipango ya Udhamini kwa Wanafunzi walio na Ulemavu** .......... **33**

Wakati Taarifa Inatolewa

# Maelezo ya Jumla

## Idhini ya Mzazi Baada ya Ufahamu

Idhini ya mzazi baada ya ufahamu inamaanisha kuwa wewe na/au mzazi mbadala aliyeteuliwa na wilaya anatoa ruhusa, katika maandishi, ili wilaya ya shule ichukue hatua. Ruhusa yako pia inamaanisha wilaya ilikupa maelezo kuhusu hatua iliyopendekezwa. Wilaya ya shule ya mtoto wako lazima ipate ruhusa hii kutoka kwako, katika maandishi, ili itekeleze shughuli fulani zinazohusiana na elimu maalum ya mtoto wako. Wilaya ya shule lazima ipate ruhusa yako iliyoandikwa:

- Kabla ya wilaya kutathmini mtoto wako kwa mara ya kwanza ili kuchunguza iwapo mtoto wako anahitaji elimu maalum na huduma husika;
- Kabla ya wilaya kuanza kutoa huduma za elimu maalum kwa mtoto wako zilizoorodheshwa kwenye mpango wake wa kwanza wa elimu wa mtu binafsi, pia inayojulikana kama IEP;
- Kabla ya wilaya kutathmini tena mtoto wako ili kuchunguza iwapo mahitaji ya mtoto wako yamebadilika;
- Kabla ya wilaya kutekeleza uchunguzi wa ziada kwa mtoto wako. Mfano ni kama vile Uchunguzi Kuhusu Tabia;
- Kabla ya wilaya kubadilisha uwekaji wa kielimu wa mtoto wako. Hatua hii haimaanishi kubadilisha eneo. Badala yake, inamaanisha kubadilisha mpango wa kielimu wa mtoto wako; na
- Kabla ya wilaya itoe maelezo kuhusu mtoto wako kwa mtu mwingine isipokuwa wale walioorodheshwa chini ya sheria ya jimbo au nchi.

### Je, Mzazi Mbadala ni Nani?

Mzazi mbadala ni mtu ambaye anaweza kuwakilisha mtoto wako aliye na ulemavu katika masuala yote kuhusiana na ustahiki na upokeaji wa huduma za elimu maalum.

Wilaya ya shule ambako unaishi huteua mzazi mbadala kila wakati jambo moja kati ya haya linatokea:

- Mzazi hawezi kutambuliwa;
- Wilaya ya shule, baada ya juhudi adilifu, imeshindwa kutambua mahali mzazi aliko;
- Mtoto ni kijana bila makazi na asiyeandama na mtu yeyote, au
- Mtoto ako chini ya mlezi wa kisheria.

**Idhini ya Mzazi Baada ya Ufahamu Haihitajiki Wakati Mojawapo ya Yafutayo Yanafanyika:**

- Wilaya inakagua maelezo yaliyopo ya mwanafunzi kama sehemu ya mchakato wa tathmini/tathmini nyingine; au
- Wilaya hupea mtoto wako tathmini ambayo wanafunzi wote hufanya.



**Ili Utoe Idhini Yako ya Mzazi Baada ya Ufahamu, Wilaya:**

- Inapaswa kuhakikisha imetumia lugha yako ya asili, au mbinu zingine za mawasiliano ambazo unaelewa, ili kukupa maelezo yote unayohitaji ili kufanya maamuzi;
- Inapaswa kuhakikisha kuwa unaelewa na unakubali katika maandishi kuwa wilaya itatekeleza shughuli na kwamba idhini yako inaelezea shughuli hio, na pia rekodi zozote za mtoto wako ambazo zitashirikiwa na wengine na kutambua watu hao;
- Inapaswa kuhakikisha kuwa unaelewa kuwa unatoa idhini kulingana na chaguo lako na unaweza kubadili mawazo yako wakati wowote;
- Inapaswa kuhakikisha kuwa unaelewa kuwa ikiwa utaondoa idhini yako, wilaya haitatendua hatua yoyote ambayo ilifanya kati ya wakati ulipotoa ruhusa na wakati ulipoiondoa.

**Kuondoa Idhini**

Kuondoa idhini inamaanisha unaondoa ruhusa yako. Unaweza kuondoa idhini yako wakati wowote ikiwa utaamua kuwa huhitaji tena mtoto wako apokee huduma za elimu maalum kama zinavyotolewa kwenye IEP ya mtoto wako. Lazima ufanya hivi kwa njia ***ya maandishi***.

Kisha, wilaya ya shule yako:

- Lazima iache kutoa huduma za elimu maalum katika IEP kwa mtoto wako, lakini kabla ya kuacha kutoa huduma hizi, wilaya lazima ikupe taarifa kwa njia ya maandishi kuwa inapanga kuacha kutoa huduma. Taarifa ambayo wilaya itakupa inaitwa taarifa ya ya mapema ya maandishi. Taarifa hii ya mapema ya maandishi lazima itimize mahitaji yaliyowekwa kwenye sehemu ya Taarifa ya Mapema ya Maandishi katika ukurasa wa 9 wa mwongozo huu.

Baada ya wilaya kukupa taarifa ya mapema ya maandishi ikieleza kuwa itaacha kutoa huduma za elimu maalum kwa mtoto wako na baada ya huduma kuacha kutolewa, wilaya haitazingatia tena kuwa mtoto wako anastahiki elimu maalum na badala yake itazingatia mtoto wako kuwa mwanafunzi wa kawaida.



## Je, Mtoto Wako Anastahiki Elimu Maalum?

Kustahiki ina maana kuwa mtoto wako amegunduliwa kuwa anahitaji huduma fulani za elimu kwa sababu ya ulemavu wa aina moja au zaidi. Sheria ya Elimu kwa Watu walio na Ulemavu (IDEA) inahitaji wanafunzi walio na ulemavu kupokea elimu maalum na/au huduma husika. Ili kuzingatiwa kuwa mwanafunzi aliye na ulemavu chini ya sheria hii, mtoto wako lazima ahitaji elimu maalum na/au huduma husika kwa sababu ulemavu wake umejumuishwa kwenye aina moja au zaidi za ulemavu ufuatao:

- Ulemavu wa kiakili;
- Kasoro ya kusikia;
- Matatizo ya lugha au matamshi;
- Kasoro ya kuona;
- Kuchanganyikiwa;
- Kasoro na magonjwa ya mifupa;
- Ugonjwa wa akili wa watoto;
- Majeraha ya ubongo kutokana na mgongano;
- Kasoro nyingine ya kiafya;
- Ulemavu mahususi wa kujifunza;
- Uziwi;
- Uziwi-upofu;
- Ulemavu wa aina nyingi; au
- Kuchelewa katika ukuaji.

**Lugha Asili au Mbinu Zingine za Mawasiliano**

**Mikutano yote utakayohudhuria, tathmini ya mtoto wako na taarifa zote lazima zitolewe kwa njia ya maandishi au kuzungumzwa kwa lugha yako ya asili au mbinu zingine za mawasiliano unazotumia.**

**Mitihani yote na nyenzo zingine zinazotumika kutathmini mtoto wako lazima zitolewe katika lugha ya asili ya mtoto wako — au mbinu zingine za mawasiliano ambazo zitaipa wilaya maelezo sahihi kuhusu mambo ambayo mtoto anayajua na anayowezo kufanya katika masomo, ukuaji na utendaji, isipokuwa kama haiwezekani kutolewa au kusimamiwa.**

### Omba Wilaya Itathmini Mtoto Wako

Ikiwa unahisi kwamba mtoto wako huenda akawa na ulemavu ambao unaathiri elimu yake, unaweza kuiomba wilaya itathmini mtoto wako ili ibaini ikiwa anastahiki elimu maalum (aweze kuzingatiwa kuwa mtoto aliye ulemavu chini ya IDEA). Wilaya ya shule pia inaweza kukuomba wakati wowote ikiwa ungependa mtoto wako atathminiwe ikiwa wafanyakazi wa wilaya wahahisi kuwa mtoto wako anahitaji elimu maalum. Katika hali zote, baada ya wilaya ya shule kupata ruhusa yako (idhini) kwa njia ya maandishi, lazima ikamilishe tathmini ya mwanzo (kwanza) ndani ya siku 60 za kalenda.

### Ikiwa Mtoto ako Chini ya Mlezi wa Kisheria

Ikiwa mtoto yuko chini ya ***ya mlezi wa kisheria*** na haishi na mzazi wake, wilaya ya shule haihitaji idhini kutoka kwa mzazi kwa tathmini ya mwanzo ili kubaini ikiwa mtoto ana ulemavu katika hali zifuatazo:

- Ikiwa, licha ya juhudi zinazowezekana, wilaya ya shule imeshindwa kutambua alipo mzazi wa mtoto;
- Haki za wazazi zimesimamishwa; au
- Haki za wazazi zimetolewa na hakimu kwa mtu ambaye ameidhinisha tathmini ya mwanzo.

## Tathamini Huru za Kielimu (almaarufu IEE)

Tathmini huru ya kielimu (IEE) pia inajulikana kama tathmini ya nje. Wilaya ya shule italipia tathmini hii ya nje ikiwa tu tayari imefanya tathmini yake kwa mtoto wako na haujakubaliana na matokeo ya wilaya. Madhumuni ni kugundua ikiwa mtoto wako anahitaji elimu maalum, au ataendelea kuhitaji elimu maalum. Mtu anayetathmini mtoto wako katika tathmini ya nje hawezi kufanya kazi na wilaya ya shule ya mtoto wako. Wewe, kama mzazi una haki, wakati wowote, kuratibu na kulipia tathmini ya nje kwa ajili ya mtoto wako. Baada yakutokubaliana na tathmini ya wilaya kuhusu mtoto wako na kuomba tathmini ya nje, wilaya yako lazima itekeleze mojawapo wa hatua zifuatazo bila kuchelewa:

- Wilaya ya shule lazima ikujulishe kuhusu mahali unapoweza kupata tathmini ya nje kwa ajili ya mtoto wako na ikufahamishe kuhusu mbinu zinazohitajika ili wilaya iweze kuilipia. Baada ya wilaya kukubali na upate tathmini ya nje, wilaya lazima ilipie gharama; au
- Wilaya lazima iwasilishe ombi katika Ofisi ya Idara ya Elimu ya Ohio kwa Watoto wa Kipekee kwa ajili ya mchakato wa utatuzi wa mgogoro (angalia ukurasa wa 21) kwa sababu haikubaliani na ombi lako la kutaka tathmni ya nje. Hili linaweza kutokea kwa sababu wilaya inahisi kuwa tathmni yake ya mtoto wako ilikuwa sahihi.


### Vigezo vya Tathmini za Nje

Vigezo ambavyo vinatumika kwa tathmini ambazo zinafanywa na wilaya pia vitatumika kwa tathmini za nje ambazo wazazi wanapanga na wilaya kulipia. Vigezo hivi ni pamoja na mahali mtoto wako atakwenda kwa ajili ya tathimini na uzoefu wa mtu atakayechunguza mtoto wako. Wilaya lazima ilipie gharama yote ya tathmini ya nje ambayo inatimiza vigezo vya wilaya.

Ikiwa utaomba tathmni ya nje kwa ajili ya mtoto wako, huenda wilaya ikakuomba ueleze***sababuyako*** ya kutokubaliana na tathmini ya wilaya ya mtoto wako (yaani, sababu zako za kutaka tahmini ya nje), lakini sio lazima ueleze hii isipokuwa kama unataka kufanya hivyo. Una haki ya tathmini moja tu ya nje inayolipiwa na wilaya, kwa kila wakati wilaya inatathmini mtoto wako na ukose kukubaliana na matokeo ya tathmini ya wilaya.

Baada ya mtoto wako kufanyiwa tathmini ya nje ambayo inatimiza vigezo vya wilaya, bila kujali aliyeilipia, wilaya lazima izingatie matokeo ya tathimini hiyo na ibaini jinsi itakavyotoa elimu inayofaa ya umma kwa mtoto wako bila malipo (almaarufu FAPE).

**Chati Ifuatayo Inaonyesha Hali Tofauti ambazo Hutokea Unapoomba Tathmini ya Nje**



### Muhtasari

Wilaya ya shule lazima ikupe taarifa ya maandishi(inayojulikana kama taarifa ya mapema ya maandishi) ndani ya kipindi kinachofaa cha wakati kabla ipendekeze au ikatae kuchukua hatua fulani. Hatua hizi ni pamoja na wilaya kuanzisha au kubadilisha utambulisho, tathmini au uwekaji katika elimu kwa mtoto wako au utoaji wa elimu inayofaa ya umma bila malipo kwa mtoto wako. Taarifa ya mapema ya maandishi ni fomu inayohitajika ya elimu maalum.

### Yaliyomo kwenye Taarifa ya Mapema ya Maandishi

Taarifa ya mapema ya maandishi lazima itoe maelezo ya kutosha ili uweze kushiriki katika maamuzi ya huduma za kielimu za mtoto wako ukiwa na ufahamu wa kutosha. Hususan, taarifa ya mapema ya maandishi lazima ijumuishe maudhui fulani, kama ilivyoelezwa kwenye kisanduku kilicho kwenye ukurasa huu.

### Taarifa ya Mapema ya Maandishi katika Lugha Inayoeleweka

Taarifa ya mapema ya maandishi lazima itolewe katika lugha ambayo inaeleweka na umma na pia lazima iandikwe katika lugha yako ya asili au mbinu zingine za mawasiliano isipokuwa kama haiwezekani kufanya hivyo.

Ikiwa luhga ya asili ya mzazi au mbinu zingine za mawasilianao ***sio***lugha inayoandikwa, basi wilaya inahitaji kuchukua hatua za kutafsiri kwa njia ya matamshi taarifa ya mapema ya maandishi, au kwa njia nyingine inayoeleweka, katika lugha ya asili ya mzazi au mbinu nyingine ya mawasiliano. Wilaya itahitaji kuhakikisha kuwa inaweza kuonyesha, katika maandishi, kwamba taarifa ya mapema ya maandishi ilitafsiriwa inavyofaa na kuwa mzazi alielewa maudhui yaliyomo.

**Taarifa ya Mapema ya Maandishi Lazima Ijumuishe:**

- Maelezo kuhusu hatua iliyopendekezwa au kukataliwa na wilaya;
- Ufafanuzi kuhusu sababu za wilaya ya shule kupendekeza au kukataa kuchukua hatua;
- Maelezo kuhusu kila utaratibu wa tathmini, rekodi au ripoti ambazo shule ilitumia ili kufanya maamuzi;
- Taarifa kuwa wazazi wana ulinzi chini ya ulinzi wa taratibu za IDEA, na ikiwa taarifa sio rufaa ya mwanzo ya tathmini, njia ambayo mzazi anaweza kupata maelezo kuhusu ulinzi wa taratibu;
- Vyanzo ili wazazi waweze kuwasiliana ili wasaidiwe kuelewa mahitaji ya IDEA;
- Maelezo kuhusu chaguo zingine ambazo timu ya IEP ilizingatia na sababu za kukataliwa kwa chaguo hizo;
- Maelezo kuhusu vipengele vingine vilivyofaa katika pendekezo au kukataa kwa wilaya.



# Rekodi za Kielimu

## Ufikiaji wa Rekodi

Sheria ya Haki na Faragha ya Kielimu kwa Familia(FERPA) ni sheria ya nchi ambayo inatoa haki fulani kwa wazazi ili kuchunguza na kukagua rekodi za kielimu za watoto wao. Haki chini ya FERPA zinahamishwa kutoka kwa mzazi hadi kwa mwanafunzi wakati mwanafunzi anatimiza umri wa miaka 18 au anaanza kuhudhuria shule ya baada ya sekondari (k.m. chuo au chuo kikuu), yoyote inayofanyika kwanza.

### Je, Rekodi za Kielimu Ni Nini?

Kama maelezo fulani kuhusu mwanafunzi yanalindwa na FERPA inategemea kama kipengee kinamaanisha ya rekodi kielimu. FERPA inafafanua rekodi za kielimu kuwa:

1. Rekodi ambazo zinahusiana moja kwa moja na mwanafunzi mahususi. Wakati mwingine shule inarejelea hii kama maelezo ya kumtambulisha mtu; na
2. Rekodi ambazo zinahifadhiwa na shirika au taasisi ya kielimu (kwa mfano, wilaya ya shule yako) au na mshirika anayewakilisha shirika hilo.

### Utunzaji na Usiri wa Rekodi

Rekodi za kielimu zinaweza kutunzwa kwa njia mbalimbali. Baadhi ya mifano ni:

- Maandishi yaliyoandikwa kwa mkono;
- Chapisho;
- Kompyuta;
- Kanda ya video au sauti; au
- Kanda ya filamu, filamu ndogo au filamu ya picha.

Rekodi za mwanafunzi ni za siri, kumaanisha kuwa ni za ***faragha***. Wilaya ya shule au shirika lazima zilinde faragha ya rekodi za mtoto wako wakati zinakusanya, kuhifadhi, kuzitoa au kuziharibu.

### Kukagua Rekodi za Mtoto Wako

Wilaya ya shule lazima ikuruhusu ukague rekodi za kielimu za mtoto wako bila ucheleweshaji usiotakikana na kabla ya mkutano wowote wa timu ya IEP au mchakato wowote unaotarajiwa ambapo unahusika. Wilaya haiwezi kusubiri zaidi ya siku 45 kutoka tarehe ulipotuma ombi ili ikiruhusu uangalie rekodi.

Una haki ya kukagua tu maelezo kwenye rekodi ambayo yanahusu mtoto***wako***. Una haki ya kuomba shule itoe ufafanuzi kuhusu rekodi za mtoto wako.  Una haki ya kuwa na mtu, ambaye anatenda kwa niaba yako, achunguze rekodi, (kama vile rafiki au mwanasheria).

Wilaya inaweza kukupa nakala za rekodi za mtoto wako; hata hivyo wilaya ***lazima***ikupe nakala ikiwa kutofanya hivyo kutakuzuia utekeleze haki yako ya kukagua rekodi. Una haki wakati wote ya kupokea nakala za rekodi ikiwa utalipia gharama.

**Maelezo ya Kumtambulisha Mtu yanajumuisha:**

- **Jina la mtoto wako;**
- **Jina la mwanafamilia;**
- **Anwani ya mtoto wako au anwani ya familia;**
- **Utambulisho wa kibinafsi, kama vile nambari ya usalama wa jamii ya mtoto wako, nambari ya mwanafunzi au rekodi ya bayometriki;**
- **Njia zingine zisizo za moja kwa moja za kutambua mtoto wako, kama vile tarehe ya kuzaliwa, mahali pa kuzaliwa, jina la mama, jamii au kabila;**
- **Maelezo mengine ambayo, peke yake au kwa kujumuishwa pamoja, yanahusishwa au yanaweza kuhusishwa na mwanafunzi mahususi ambayo yanaweza kuruhusu mtu aliye katika jumuiya ya shule, ambaye hana ufahamu wa kibinafsi wa hali zinazofaa, kutambua mwanafunzi kwa usahihi;**
- **Maelezo yalioombwa na mtu ambaye shule inaamini ana ufahamu wa utambulisho wa mtoto wako; au**
- **Mifano mingine kama inavyofafanuliwa na FERPA.**



### Mabadiliko kwenye Rekodi za Kielimu

Una haki ya kuomba wilaya ya shule ibadilishe maelezo yasiyo sahihi au yanayopotosha kwenye rekodi za kielimu za mtoto wako. Shule ya mtoto wako haihitajiki kubadilisha rekodi za kielimu kulingana tu na ombi lako (kwa sababu tu umeomba hilo), lakini shule lazima ***izingatie*** ombi lako. Ikiwa shule itaamua kutobadilisha rekodi ya mtoto wako kama ulivyoomba, shule lazima ikujulishe kuwa una haki ya utatuzi wa mgogoro ili kujadili kuhusu suala.

Baada ya kikao cha maamuzi, ikiwa shule bado inaamua kutobadilisha rekodi ya kielimu, una haki ya kujumuisha taarifa yako kuhusu suala hilo kwenye rekodi ya mtoto. Taarifa hii inatasalia kama sehemu ya rekodi ya mtoto wako. Chaguo la kuandika taarifa itakayowekwa kwenye rekodi ya mtoto wako linatumika ***tu ikiwa rekodi zinajumuisha maelezo yasiyo sahihi***. Hufai kutumia taarifa kama hio ili kupinga alama ambayo mtoto wako alipata, maoni ya kibinafsi au uamuzi muhimu uliofanywa na shule kuhusu mtoto wako.

### Kushiriki Rekodi za Kielimu

Kwa kawaida, wilaya ya shule lazima ipate ruhusa yako kwa njia ya maandishi ikiwa inataka kushiriki rekodi za kielimu ambazo zinatambua mtoto wako na mtu mwingine isipokuwa wewe. Hata hivyo, kuna hali ambapo ruhusa yako haihitajiki. Ili upate maelezo zaidi kuhusu wakati wilaya ***haihitaji*** kupata ruhusa yako ya maandishi ili kushiriki rekodi, angalia mwongozo wa jumla wa FERPA kwa wazazi katika tovuti ya Idara ya Elimu ya Marekani katika www.ed.gov.



# Utatuzi wa Mgogoro

## Mchakato wa Utatuzi wa Mgogoro

Ikiwa una wasiwasi kuhusu elimu ya mtoto aliye na ulemavu, hatua ya kwanza ni kushirikiana na wilaya ya shule yako. Kuanza, wasiliana na mwalimu wa mwanafunzi au mkurugenzi wa elimu maalum katika wilaya yako. Julisha mtu huyo kuhusu wazo lako. Ikiwa wewe na wilaya hamkubaliani kuhusu wasiwasi wako, kuna njia mnazoweza kutumia ili kushirikiana kusuluhisha tatizo.

Michakato hii ina majina rasmi ambayo wilaya ya shule huenda ikatumia, lakini mwongozo huu utakusaidia uelewe ufafanuzi wa majina hayo na jinsi ambavyo wewe na shule mnaweza kumsaidia mtoto wako. Sehemu ifuatayo inaeleza michakato au mbinu hizi ambazo unaweza kutumia ili kushirikiana na wilaya yako.

### Ukaguzi wa Usimamizi

Ikiwa hutakubaliana na uamuzi wa wilaya ya shule yako kuhusiana na elimu ya mtoto wako aliye na ulemavu, unaweza kuwasilisha lalamiko kwa usimamizi wa wilaya. Kutokana na hilo, msimamizi (au mwakilishi) wa wilaya atatekeleza ukaguzi wa usimamizi. Ukaguzi huu huenda ukajumuisha mchakato wa ukaguzi wa usimamizi.

Ukaguzi na mchakato wa ukaguzi wa usimamizi, ikiwa mojawapo inafanyika, lazima ifanyike katika wakati na mahali adilifu kwa kila mshirika. Wewe na wilaya mnaweza kualika watu wengine kuhudhuria ukaguzi na mchalato wa ukaguzi wa usimamizi. Kwa mfano, unaweza kualika wanafamilia wengine au rafiki, mtu aliye na ufahamu kuhusu elimu maalum au mwanasheria. Ikiwa mtoto wako anafunzwa katika mpango wa elimu unaotekelezwa na bodi ya ulemavu wa ukuaji ya kaunti au shiriki lingine la elimu ya umma, wilaya lazima ijadiliane na bodi au shirika hilo kwa ajili ya mchakato wa ukaguzi wa usimamizi.

Katika ukaguzi wa hali, juhudi zote zinapaswa kufanyika ili kusuluhisha hali hii ya kutofautiana kuhusu elimu ya mtoto. Msimamizi (mwakilishi) atasikiliza kila upande wa wahusika wanaotofautiana na kufanya uamuzi. Baada ya kufikia uamuzi, msimamizi lazima akujulishe, kwa maandishi, kuhusu uamuzi. Jambo hili lazima lifanyike ndani ya siku 20 kutoka wakati ulipojulisha wilaya kuhusu wasiwasi wako.

### Michakato ya Ziada Unayoweza Kujaribu Kutumia

Ikiwa umekamilisha mchakato huu na wewe pamoja na wilaya ya shule bado mnatofautiana kuhusu jinsi ya kusuluhisha tatizo, kuna michakato mingine unayoweza kujaribu. Ingawa huhitajiki kuomba mchakato wa ukaguzi wa usimamizi kabla ya kuanza michakato mingine ya utatuzi wa mgogoro, inahimizwa ufanye hivyo. Kuna chaguo za ziada ambazo unaweza kutumia ili kusuluhisha tatizo. Ofisi ya Idara ya Elimu ya Ohio ya Watoto wa Kipekee inaweza kuhusika na kukusaidia katika ombi lako kwa kutoa zana za ziada ili kusuluhisha wasiwasi wako. Mahirika yafuatayo pia yanaweza kukusaidia:

- Timu ya Usaidizi ya Jimbo katika eneo lako (nambari ya Eneo _______________) kupitia (nambari ya simu _____________________________). Mshauri wa mzazi na familia katika Timu ya Usaidizi ya Jimbo atashirikiana nawe.
- Mshauri wa mzazi katika eneo, ikiwa anapatikana katika wilaya ya shule yako.
    - Mshauri wa mzazi hutoa maelezo na usaidizi kwa familia za mtoto aliye na ulemavu na wilaya za shule. Mshauri wa mzazi ni mfanyakazi wa wilaya na pia mzazi wa mtoto aliye na ulemavu.
    - Kwa maelezo zaidi wasiliana na _____________________________________________________.
- Muungano wa Ohio kwa Elimu ya Watoto walio na Ulemavu (OCECD)
    - OCECD ni shirika lisilo la faida linalopatikana kote nchini ambalo linahudumia familia za watoto wachanga, watoto na vijana walio na ulemavu katika Ohio, na walimu na mashirika ambayo hutoa huduma hizi. Mipango ya OCECD husaidia wazazi kupata ufahamu na kuwa wawakilishi wenye ufanisi wa watoto wao katika mazingira yote ya kielimu.
    - Kwa maelezo zaidi, wasiliana na OCECD kupitia (740) 382-5452 au utembelee tovuti ya OCECD katika: www.ocecd.org.

## Utatuzi wa Mapema wa Lalamiko

Utatuzi wa mapema wa lalamiko ni wakati unapojaribu kusuluhisha tofauti kati yako na wilaya ya shule kwa njia isiyo rasmi na kwa kawaida kabla ya kuanza kutumia chaguo zingine za utatuzi wa mgogoro. Mtu kutoka Ofisi ya Idara ya Elimu ya Ohio kwa Watoto wa Kipekee atashirikiana nawe ili kukusaidia kusuluhisha maswali na wasiwasi wako kuhusu elimu ya mtoto wako.

Idara ya Elimu ya Ohio inahimiza utatuzi wa mapema wa lalamiko kabla uombe michakato zaidi rasmi, kama vile malalamiko ya maandishi au mchakato wa utatuzi wa mgogoro. Unaweza kuwasiliana na mtu katika Ofisi ya Idara ya Elimu ya Ohio kwa Watoto wa Kipekee ili asaidie kusuluhisha maswali na wasiwasi wako kuhusu elimu ya mtoto wako. Ili kuwasiliana na mtu kuhusu utatuzi wa mapema wa lalamiko, tafadhali wasiliana na Idara:

- Kupitia simu: (614) 466-2650, au simu isiyolipishwa (877) 644-6338; au
- Kupitia barua pepe: exceptionalchildren@education.ohio.gov.

## Msaada

Ikiwa una wasiwasi kuhusu tathmini au tathmini nyingine ya mtoto wako katika elimu maalum, au kuhusu Mpango wa Elimu wa Mtu Binafsi (IEP), unaweza kutumia chaguo ambalo linajulikana kama msaada.

Msaada ni wakati unaomba Idara ifanye mipango ili msaidizi ahudhurie mkutano wa tathmini ya mtoto wako au timu ya IEP (wewe pia ni mwanachama wa timu hii). Wilaya ya shule pia inaweza kuomba Idara itoe msaidizi katika mojawapo wa mikutano hii inayohusiana na elimu maalum ya mtoto wako. Wewe pamoja na wilaya lazima mkubaliane kuwa msaidizi atahudhuria mkutano..

### Madhumuni ya Msaada

Msaada hufanyika katika mkutano wa timu, kama vile mkutano wa timu ya mpango wa elimu wa mtu binafsi, mkutano wa kupanga tathmini au mkutano wa timu ya tathmini. Msaidizi ni mtu asiyehusika moja kwa moja, ambaye haegemei upande wowote na sio mwanachama wa timu na hafanyi maamuzi kwa ajili ya timu. Kuwa na msaidizi husaidia timu ifanye kazi kwa ufanisi na kuzingatia mwanafunzi. Wasaidizi ni wapatanishi wataalam waliopata mafunzo kutoka kwa Ofisi ya Watoto wa Kipekee katika michakato ya elimu maalum.

Unaweza kuomba msaada wakati wowote. Baada ya kuomba, wewe pamoja na wilaya ya shule lazima mkubali kuwa mtashiriki. Ikiwa nyote mnakubali, Ofisi ya Watoto wa Kipekee itakupa chaguo za msaidizi atakayeongoza mkutano. Ikiwa wewe na wilaya hamkubaliani ni nani atakuwa msaidizi, ofisi itawachagulia mmoja. Hakuna gharama utakayotozwa wewe au wilaya kwa ajili ya msaada.

### Msaidizi:

- Atasalia kuwa mtu asiyehusika moja kwa moja asiyeegemea upande wowote (hapendelei upande au kufanya kazi kwa ajili yako au wilaya);
- Ni mtaalam aliye na mafundisho kama ***mpatanishi*** (mtu aliyehitimu ambaye husaidia kutatua migogoro);
- Amepata mafundisho kuhusu na ana ufahamu wa sheria na mahitaji ya elimu maalum;
- Sio sehemu ya IEP ya mtoto wako au timu ya tathmini;
- Hafanyi maamuzi, lakini anaongoza timu ili kupata suluhisho;
- Husaidia kuleta uwazi katika mazungumzo kati yako na wilaya;
- Huhakikisha mkutano unaendelea kama ilivyopangwa na huhakikisha kila mtu ana heshimu mchakato; na
- Huhakikisha timu inazingatia mtoto na mahitaji ya mtoto.



**Mambo Makuu ya Kukumbuka Kuhusu Suluhisho:**

- **Msaada huwa kwa hiari.**
  - Mzazi pamoja na wilaya ya shule lazima wakubali kuwa sehemu ya mchakato. Ikiwa mzazi na wilaya watakubaliana kuwa na msaidizi katika mkutano, hii haimanishi kuwa ni lazima ukubaliane na wilaya wakati wa mkutano au ukubaliane na matokeo ya mkutano. Wazazi kila wakati wanaruhusiwa kuwa na maoni yao.
- **Makubaliano yoyote yanayofikiwa wakati wa mkutano wa msaada yanaanza kutumika kwa jumla. Hili linamaanisha kuwa mzazi pamoja na wilaya ya shule lazima wafuate makubaliano baada ya uamuzi kufanywa kwa pamoja.**
  - Hati yoyote ambayo mzazi au wilaya inasaini kuhusu tathmini ya mtoto wako au IEP ni muhimu tu kama hati zilizotiwa saini katika mkutano mwingine wowote wa IEP au timu ya tathmini.

Kwa maelezo zaidi kuhusu msaada, tembelea tovuti ya Idara ya Elimu ya Ohio katika: [education.ohio.gov](education.ohio.gov) na utafute ***msaada.***

### Kutuma Ombi la Msaada

Wasiliana na mkurugenzi wa elimu maalum katika wilaya ya shule yako ili kujua ikiwa wilaya inapanga kushiriki katika mchakato huu, ________________________________ katika __________________________________. Baada ya washirika wote kukubali kushiriki katika msaada, tafadhali wasiliana na Ofisi ya Idara ya Elimu ya Ohio ya Watoto wa Kipekee:

- Kupitia simu: (614) 466-2650, au simu isiyolipishwa (877) 644-6338; au
- Kupitia barua pepe: [exceptionalchildren@education.ohio.gov](mailto:exceptionalchildren@education.ohio.gov).

## Upatanisho

Upatanisho ni wakati mzazi na wilaya ya shule wanakubaliana kuwa na mtaalam asiyehusika moja kwa moja na asiyeegemea upande wowote ahudhurie mkutano ili awasaidie kufikia makubaliano kuhusu elimu ya mwanafunzi aliye na ulemavu au mwanafunzi ***anayeshukiwa*** kuwa na ulemavu. Mtu asiyehusika noja kwa moja inaamanisha kuwa mtu huyu, pia anayejulikana kama mpatanishi, hapendelei upande wowote na hafanyi kazi au kuwakilisha kwa niaba ya mzazi au wilaya. Upatanisho ni chaguo moja kwa wazazi na wilaya wakati wowote mnapotofautiana kuhusu elimu maalum ya mtoto wako.



### Upatanisho Haulipishwi na Unaweza Kuombwa Wakati Wowote

Upatanisho unaweza kuombwa wakati wowote. Baada ya kuomba upatanisho, wewe pamoja na wilaya lazima mkubali kushiriki katika mchakato. Ikiwa nyote mnakubali kushiriki, Ofisi ya Watoto wa Kipekee itatoa chaguo za wapatanishi wa kuongoza mkutano wa upatanishi. Ikiwa wewe na wilaya mmeshindwa kukubaliana kuhusu nani atakuwa mpatanishi, OEC itawapea mmoja. Mpatanishi hawezi kuwaeleza jinsi mnavyopaswa kusuluhisha suala kuhusu elimu maalum kwa mtoto wako. Bali, mpatanishi husaidia pande zote kujadiliana kuhusu wasiwasi unaohusu mtoto wako na kupata suluhisho.

Ikiwa utaamua kutuma lalamiko rasmi au kuomba mchakato wa utatuzi wa mgogoro (angalia kurasa za 17-25), Idara ya Elimu ya Ohio itakuomba uzingatie upatanisho kama hatua ya kwanza. Hakuna gharama zozote ambazo wewe au wilaya itatozwa kwa ajili ya upatanisho.

## Muhtasari wa Mchakato wa Upatanisho

### Ombi la Upatanisho

Wewe au wilaya ya shule mnaweza kuomba Idara ya Elimu ya Ohio kutoa upatanisho wakati wowote. Ikiwa utatuma lalamiko au uombe mchakato wa utatuzi wa mgogoro, Idara itatoa upatanisho kama hatua ya kwanza. Wewe na wilaya lazima mkubali kutumia mpatanishi.

### Chagua Mpatanishi na Ratibu Mkutano

Mpatanishi ni mtu asiyehusika moja kwa moja asiyeegemea upande wowote. Wewe na wilaya ya shule lazima mkubali kutumia mpatanishi. Mpatanishi ataratibu mkutano haraka iwezekanavyo. Idara inalipa mpatanishi.

### Mkutano wa Upatanisho

Wewe pamoja na wilaya ya shule mnashiriki wasiwasi wenu. Mpatanishi anawasaidia kutatua mgogoro na kufikia makubaliano ya mwisho, yaliyoandikwa. Kwa jumla, hakuna jambo linalozungumziwa wakati wa mkutano linalopaswa kushirikiwa nje ya mkutano au kutumiwa katika kesi za kisheria za siku za usoni, isipokuwa katika hali zisizo za kawaida.

### Makubaliano Yamefikiwa

Makubaliano ya maandishi huwa yanatumika na mzazi pamoja na wilaya ya shule lazima wayatilie saini. Kutumika inaamanisha kuwa mzazi na shule lazima wafuate makubaliano na mahakama inaweza kuyatekeleza.

### Makubaliano Hayajafikiwa

Ikiwa makubaliano hayatafikiwa wakati wa upatanisho, na ulitoa lalamiko la ukiukwaji wa sheria za jimbo, basi Ofisi ya Watoto wa Kipekee itasuluhisha lalamiko. Ikiwa makubaliano hayatafikiwa wakati wa upatanisho na uliomba mchakato wa utatuzi wa mgogoro, basi usikilizaji wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro utafuata.



**Mpatanishi:**

- Atasalia kuwa mtu asiyehusika moja kwa moja asiyeegemea upande wowote (hapendelei upande au kufanya kazi kwa ajili yako au wilaya);
- Haruhusiwi kufanya maamuzi. Badala yake, mpatanishi hukusaidia pamoja na wilaya ya shule ili kutatua suala kuhusiana na elimu ya mtoto wako;
- Anafanya kazi pamoja na wewe na wilaya ya shule ili kuamua kuhusu makubaliano ya upatanisho yaliyoandikwa;
- Huhakikisha mkutano wa upatanisho unaendelea kama ilivyopangwa na huhakikisha kila mtu anaheshimu mchakato;
- Huhakikisha kila mshirika anazingatia mwanafunzi na mahitaji ya mwanafunzi;
- Husaidia kuanzisha mazungumzo kati yako na wilaya.

**Mambo Makuu ya Kukumbuka Kuhusu Upatanisho**

- **Upatanisho huwa wa kujitolea.**
  — Mzazi pamoja na wilaya ya shule lazima wakubali kuwa sehemu ya mchakato. Ikiwa mzazi na wilaya watakubali kushiriki katika upatanisho, hii haimaanishi kuwa ni lazima ukubaliane na wilaya wakati wa mkutano au ukubaliane na matokeo ya mkutano.

- **Upatanisho hutekelezwa kwa usiri.**
  — Mambo yote yanayozungumziwa wakati wa mkutano wa upatanisho kwa ujumla huwa ya usiri (faragha) na hayawezi kutumiwa baadaye, isipokuwa katika hali zisizo za kawaida.

- **Makubaliano yote ya maandishi yanayofikiwa wakati wa upatanisho yanatumika kwa ujumla. Hili linamaanisha kuwa mzazi pamoja na wilaya ya shule lazima wafuate makubaliano baada ya uamuzi kufanywa kwa pamoja.**
  — Hati yoyote ambayo mzazi au wilaya inasaini kuhusu tathmini ya mtoto wako au IEP ni muhimu tu kama hati zilizotiwa saini katika mkutano mwingine wowote wa IEP au timu ya tathmini.

**Kutuma Ombi la Upatanisho**

Wasiliana na mkurugenzi wa elimu maalum katika wilaya ya shule yako ili kujua ikiwa wilaya inapanga kushiriki katika mchakato huu, ________________________________ katika________________________________. Baada ya washirika wote kukubali kushiriki katika upatanisho, tafadhali wasiliana na Ofisi ya Idara ya Elimu ya Ohio kwa Watoto wa Kipekee:

- Kupitia simu: (614) 466-2650, au simu isiyolipishwa (877) 644-6338; au
- Kupitia barua pepe: exceptionalchildren@education.ohio.gov.



## Kuandikisha Lalamiko la Ukiukwaji wa Sheria ya Jimbo

Chaguo lingine unaloweza kutumia, ikiwa una wasiwasi kuhusu elimu maalum kwa mtoto wako, ni kuandikisha lalamiko la ukiukwaji wa sheria ya jimbo kwa njia ya maandishi dhidi ya wilaya ya shule au shirika lingine la umma na kuwasilisha lalamiko hili katika Ofisi ya Idara ya Elimu ya Ohio ya Watoto wa Kipekee.

### Hakuna Gharama Inayotozwa kwa Kuandikisha Lalamiko

Hakuna gharama inayotozwa kwa kuandikisha lalamiko. Mchakato wa kuandikisha lalamiko la ukiukwaji wa sheria ya jimbo kwa ujumla husuluhisha tatizo haraka kuliko mchakato wa utatuzi wa mgogoro na una pingamizi (makabiliano) chache ukilinganisha na mchakato wa utatuzi wa mgogoro. Ili kuandikisha lalamiko la ukiukwaji wa sheria ya jimbo, lazima utume lalamiko lako ulilosaini, la maandishi (nakala halisi) kwa Ofisi ya Watoto wa Kipekee, na lazima utume ***nakala*** ya lalamiko moja kwa moja kwa wilaya ya shule.

Lalamiko lako lazima lijumuishe taarifa kuhusu ukiukwaji unaodaiwa wa mahitaji ya elimu maalum ya nchi au jimbo (ukiukwaji unaodaiwa wa Sheria ya Elimu kwa Watu walio na Ulemavu au Viwango wa Kufanya Kazi vya Ohio kwa Elimu ya Watoto walio na Ulemavu). Lalamiko sio lazima lijumuishe jina au kurejelea sheria mahususi, lakini linahitaji kueleza hatua iliyotekelezwa au kukosa kutekelezwa na wilaya ambayo unaamini ilikiuka mahitaji ya elimu maalum. Pia, lazima ujumuishe mambo bayana katika lalamiko ili kuelezea sababu unayoamini wilaya ilikiuka mahitaji ya elimu maalum.

### Ukaguzi wa Malalamiko ya Ukiukwaji wa Sheria ya Jimbo

Ofisi ya Watoto wa Kipekee itaikagua, na ikihitajika, ichunguze lalamiko lililowasilishwa kwa njia inayofaa na kubaini ikiwa wilaya ya shule imekiuka mahitaji ya elimu maalum kuhusiana na elimu ya mtoto wako. Pia, mtu asiyehusika moja kwa moja - yaani, mtu ambaye sio wewe, au shirika au taasisi na sio wilaya ya shule - anaweza kuwasilisha lalamiko la ukiukwaji wa sheria ya jimbo kupitia Idara ikiwa anaamini kuwa wilaya imekiuka mahitaji ya elimu maalum kuhusiana na mwanafunzi.

Lalamiko la ukiukwaji wa sheria ya jimbo linaweza kuwasilishwa kupitia Idara wakati wowote ndani ya ***mwaka mmoja*** kutoka wakati ukiukwaji unaodaiwa wa elimu maalum. Lalamiko lolote ambalo linadai ukiukwaji ambao ulifanyika zaidi ya mwaka mmoja kutoka tarehe ambayo lalamiko liliwasilishwa halitachunguzwa/kusuluhishwa.

### Jinsi ya Kuwasilisha Lalamiko Rasmi la Ukiukwaji wa Sheria ya Jimbo

Iwapo ungependa kuwasilisha lalamiko rasmi la ukiukwaji wa sheria ya nchi kuhusiana na elimu maalum, unapaswa:

- Kujaza fomu ya lalamiko la ukiukwaji wa sheria ya jimbo na uitume kwa Ofisi ya Idara ya Elimu ya Ohio kwa Watoto wa Kipekee; au
- Uandike barua ya lalamiko; au
- Upigie simu mfanyakazi wa Ofisi ya Idara ya Watoto wa Kipekee kupitia 1-877-644-6338 na kuomba fomu ya malalamiko, ambayo utajaza na kurudisha kwa Idara.



### Mahali Utatuma Lalalamiko Lako

Lalamiko lako lazima litumwe kwazote ***mbili*** Ofisi ya Idara ya Elimu ya Ohio ya Watoto wa Kipekee na kwa msimamizi wa wilaya ya shule kwa wakati ule ule.

Tuma lalamiko lako la mwanzo kwa:

Ofisi ya Idara ya Elimu ya Ohio
Watoto wa Kipekee

Aione: Mkurugenzi Msaidizi wa
Sehemu ya Utatuzi wa Migogoro
25 South Front Street

Mail Stop 409

Columbus, Ohio 43215-4183

### Kuahirisha

Kuahirisha humaanisha kuweka kando masuala ya malalamiko ya jimbo. Ikiwa wewe na wilaya ya shule mnahusika katika usikilizaji wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro, na wewe ama wilaya pia uandikishe malalamiko ya jimbo kuhusu masuala yale yale, Idara ya Elimu ya Ohio itaweka kando lalamiko hilo la jimbo. Yaani, Idara itangoja hadi mchakato wa utatuzi wa mgogoro ukamilike kabla ya kutatua lalamiko lako la jimbo. Ukiondoa ombi lako la mchakato wa utatuzi wa mgogoro, Idara itatoa lalamiko la jimbo kutoka katika hali ya kuahirisha na kuendelea na utatuzi wa lalamiko lako.

Ikiwa mchakato wa utatuzi wa mgogoro utafanyika na uamuzi ufanywe na ofisa msikilizaji asiyebagua (IHO), basi Idara itatoa lalamiko la jimbo kutoka katika hali ya kuahirisha ili kulitatua ikiwa tu masuala bado yamebaki katika lalamiko lako ambayo hayakuamuliwa na ofisa msikilizaji.



**Orodha ya Vitu Ambavyo Lazima Ujumuishe katika Lalamiko la Jimbo**

- **Taarifa kwamba wilaya ya shule imekiuka hitaji la elimu ya kipekee la serikali au la jimbo.**
- **Maelezo ya tatizo hilo, ukijumuisha mambo ya kweli ambayo unakadiria lalamiko lako.**
- **Maelezo yako ya mawasiliano na saini asili.**
- **Ikiwa unadai ukiukaji wa elimu ya kipekee kuhusiana na mwanafunzi fulani:**
  - **— Jina na anwani ya nyumbani ya mwanafunzi;**
  - **— Jina la shule ambayo mwanafunzi anahudhuria;**
  - **— Ikiwa ni mtoto au kijana asiye na makao (kama inavyoelezwa na Sheria ya McKinney-Vento ya Kuwasadia Wasio na Makao), maelezo ya mawasiliano ya mwanafunzi yanayopatikana na jina la shule ambayo mwanafunzi anahudhuria;**
  - **— Maelezo ya hali halisi ya tatizo, ikijumuisha mambo ya kweli yanayohusiana na tatizo hilo; na**
  - **— Utatuzi unaopendekezwa wa tatizo hilo kwa kiwango kinachojulikana na kupatikana kwa mshiriki wakati ule lalamiko linaandikishwa.**
- **Lalamiko *lazima liwe na saini yako asili, kwa hivyo huwezi kutuma lalamiko kupitia faksi au barua pepe.***
- **Malamiko ambayo hayana jina hayatakubaliwa.**

## Mchakato wa Lalamiko la Jimbo

Wakati idara inapokea lalamiko lako la jimbo, maadamu tu limeandikishwa vifaavyo, itaanza kulipitia na, kadri inavyohitajika, ichunguze ukiukwaji wa mahitaji ya elimu ya kipekee unaodaiwa. Ofisi ya Watoto wa Kipekee lazima itatue lalamiko hilo ndani ya siku 60 za kalenda kuanzia tarehe ambayo ilipokea lalamiko lako.

Kama sehemu ya mchakato wa lalamiko, Ofisi ya Watoto wa Kipekee ita:

- Pitia lalamiko lako na kuamua kama iko na mamlaka ya kutatua madai yaliyoko katika lalamiko lako;
- Kujulisha wewe na wilaya ya shule kwa njia ya maandishi kuhusu madai ambayo itatatua, pamoja na uchunguzi (kama inahitajika);
- Toa upatanisho au msaada kwako pamoja na wilaya kama njia mbadala ya kutatua lalamiko;
- Omba habari zaidi amabyo huenda ikahitaji kutoka kwako na wilaya kuhusu madai yaliyoko katika lalamiko lako;
- Pitia hati za ziada na taarifa zilizotolewa na wewe na wilaya, kuendesha mahojiano ya simu na kutembelea wilaya ya mtoto wako, kama inavyoamua ni muhimu;
- Kupatia wilaya yako fursa ya kujibu lalamiko lako na kutoa suluhisho; na
- Andika barua ya kukujulisha wewe pamoja na wilaya juu ya uamuzi wake kuhusu kama ukiukaji wa elimu ya kipekee umefanyika (baada ya kumalizia mapitio yake na uchunguzi, ikiwa inahitajika, na isizidi siku 60 za kalenda kuanzia tarehe ambayo ilipokea lalamiko lako)

### Nyongeza za Wakati

Idara inaweza kuwa na zaidi ya siku 60 za kutatua lalamiko hilo na kutoa barua ikiwa na uamuzi wake, ikiwa kutakuwa na nyongeza ya wakati. Nyongeza ya siku 60 za kutatua lalamiko la jimbo inaweza kuongezwa iwapo:

- Wewe na wilaya y shule mtakubaliana muda zaidi ili nyinyi wawili mjaribu kutatua tatizo hilo kupitia upatanisho, msaada ama njia zinginezo mbadala za kusuluhisha mgogoro; ama iwapo
- Kuna hali za kipekee (zinazobainishwa na Ofisi ya Watoto wa Kipekee kwa kuzingatia hatua kwa hatua).

### Kuandikisha ombi Visivyofaa

Ikiwa Ofisi ya Watoto wa Kipekee itabainisha kwamba hujaandikisha lalamiko la jimbo inavyofaa kwa sababu hukujumuisha habari zote zinazohitajika kuhusu suala ambalo ungetaka litatuliwe, ama ikiwa Ofisi ya

Watoto wa Kipekee haina mamlaka ya kuchunguza lalamiko hilo, Ofisi ya Watoto wa Kipekee itakutumia barua inayoelezea: mbona haitaendelea kutatua lalamiko lako, sababu ya uamuzi huo na, ikiwa inafaa, habari unazohitaji kujumuisha katika lalamiko mpya ili ionekane kwamba limeandikishwa inavyofaa.

### Kuwasilisha upya Lalamiko

Ikiwa utalazimika kuwasilisha upya lalamiko hilo likiwa na habari mpya, hakikisha umetuma lalamiko hilo kwa Idara ya Elimu ya Ohio na wilaya ya shule katika kipindi cha mwaka mmoja wakati ambapo ukiukwaji wa elimu ya kipekee unadaiwa kwamba ilitokea. Ikiwa umejumuisha masuala katika lalamiko lako ambayo Idara haina mamlaka ya kusuluhisha, itakuelekeza kwa nyenzo ili kushughulikia masuala hayo, inavyofaa.

### Kuandikisha Lalamiko

- Lalamiko liandikishwe ndani ya mwaka mmoja ambapo ukiukwaji unaodaiwa.
- Mzazi anapea Idara ya Elimu ya Ohio hati asili na nakala kwa wilaya.
- Lalamiko lidai ukiukwaji wa mahitaji ya elimu ya kipekee na kuungwa mkono na mambo ya kweli.

### Idara ya Elimu ya Ohio Inakagua Lalamiko

- Idara hutuma barua la kukubali kwamba imepoka lalamiko kwa mtu aliyeandikisha lalamiko na wilaya ya shule.
- Idara ya Elimu ya Ohio hutuma barua ya upungufu ikiwa lalamiko halijaandikishwa inavyofaa, ama ikiwa Idara haina mamlaka ya kulisuluhisha.

### Utatuzi

- Idara hupitia hati zote na kuomba hati/taarifa za ziada kama inavyohitajika.
- Idara huhoji watu wanaofaa, kama inavyohitajika.

### Idara Hutuma Barua ya Matokeo

- Idara hufanya uamuzi wa kila dai na kutambua kama kuna ukiukwaji wa elimu ya kipekee.
- Idara hutoa hatua za marekebisho ambapo wilaya imepatikana kwamba imevunja sheria.



## Kuandikisha Lalamiko la Mchakato wa Utatuzi wa Mgogoro

Mojawapo ya njia amabayo wazazi wanaweza kutatua wasiwasi fulani kuhusu elimu ya kipekee ya mtoto wao na wilaya ya shule yao ni kuwasilisha ombi la usikilizaji wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro moja kwa moja kwa wilaya, huku wakipeleka nakala kwa Idara ya Elimu ya Ohio. Ukifanya hivyo, umeandikisha lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro (pia inaitwa ombi la mchakato wa utatuzi wa mgogoro). Kuna wengine ambao wanaweza kuandikisha lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro:



- Mwanafunzi, akiwa angalau na miaka 18;
- Wilaya ya shule; ama
- Mashirika mengine ya elimu ya umma.

### Sababu za Kuandikisha

Lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro linaweza kuandikishwa kwa ajili ya wasiwasi unaohusu sehemu zifuatazo za elimu ya kipekee ya mtoto wako:

- Utambulisho wa mtoto mwenye ulemavu;
- Uchanganuzi wa mtoto mwenye ulemavu;
- Uwekaji wa kielimu wa mtoto mwenye ulemavu; ama
- Kumpa mtoto wako elimu ya umma isiyolipwa na inayofaa (FAPE).

Lalamiko la hatua zinazotarajiwa lazima lidai kuwa mahitaji ya kiserikali au ya jimbo yamekiukwa na lazima liandikishwe katika muda ***wamiaka miwili*** ya tarehe ambayo mzazi (ama shirika la elimu ya umma linalowasilisha lalamiko hilo) alijua ama alifaa kujua kuhusu madai ya ukiukwaji wa elimu ya kipekee unaodaiwa. Kila mara Idara ya Elimu ya Ohio hupokea lalamiko la usikilizaji wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro, wazazi na wilaya ya shule inayohusika lazima ipate nafasi ya kushiriki katika usikilizaji wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro. Usikilizaji wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro ni mashataka rasmi ambayo afisa msikizi asiyebagua huteuliwa na Idara kuongoza usikilizaji ili kusuluhisha lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro.

### Taarifa ya kujumuisha

Idara huandaa fomu ambayo unaweza kutumia kuomba usikilizaji wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro. Mtu au shirika la elimu ya umma linalowasilisha ombi hawalazimiki kutumia **Fomu ya Idara**, lakini mtu huyo ama shirika lazima ajumuishe taarifa hii inayohitajika anapowasilisha lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro:

1. Jina la mwanafunzi;
2. Anwani ya mwanafunzi ama maelezo ya mawasiliano;
3. Jina la wilaya ya shule;
4. Ikiwa mtoto wako hana makao, maelezo ya mawasiliano yanayopatikana ya mtoto wako na jina la shule anayohudhuria mtoto wako;
5. Maelezo ya tatizo mahususi linalohusu mtoto wako, na vile vile mambo ya kweli yanayohusu tatizo hilo; na
6. Maoni ama mapendekezo ya kutatua tatizo hilo.

Lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro lazima liwe na maelezo sawa, ya kina kama lalamiko la jimbo (angalia ukurasa wa 18), hata hivyo saini asili haihitajiki. Inaweza kupelekwa kwa wilaya ya shule na kwa Idara ana kwa ana, kupitia barua, faksi ama barua pepe. Masuala ambayo hayajajumuishwa katika lalamiko lako la mchakato wa utatuzi wa mgogoro la mwanzoni hayatapitiwa na afisa msikizi wakati wa usikilizaji wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro.

### Kurekebisha Lalamiko la Mchakato wa Utatuzi wa Mgogoro

Kurekebisha lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro ni kutengeneza upya lalamiko baada ya kuwasilishwa kwa Idara ya Elimu ya Ohio. Unaweza tu kurekebisha lalamiko lako la mchakato wa utatuzi wa mgogoro ikiwa:

- Huyo mshiriki mwingine akubali marekebisho ya lalamiko lamchakato wa utatuzi wa mgogoro kwa nia ya maandishi, na amepewa fursa ya kusuluhisha lalamiko hilo kupitia mkutano wa uamuzi (mkutano wa uamuzi umeelezwa katika ukurasa wa 23); au
- Ofisa msikilizaji asiyebagua amepeana idhini. Ofisa msikilizaji huenda akapeana idhini kama hiyo ndani ya siku tano kabla usikilizaji wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro uanze, lakini sio baada ya hapo.

## Nyakati na Mchakato wa Utatuzi wa Mgogoro

Ukiandikisha lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro dhidi ya wilaya ya shule ya mtoto wako, ndani ya siku 10 za kalenda za kupokea lalamiko lako la mchakato wa utatuzi wa mgogoro, wilaya lazima ikupe taarifa ya mapema ya maandishi ama jibu kuhusiana na ukiukwaji wa elimu ya kipekee unaodaiwa, isipokuwa tu kama wilaya tayari imepeana taarifa hiyo (ona ukurasa wa 9). Taarifa ya mapema ya maandishi ambayo wilaya hukupa lazima ijumuishe:

- Maelezo ya hatua inayohusu ombi ama lalamiko lako. Hii inaweza kuwa hatua ambayo wilaya ilitaka kuchukua ama hatua ambayo ilikataa kuchukua. Wilaya pia lazima ieleze katika jibu lake ni kwa nini shule ilitaka kuchukua hatua ama ni kwa nini ilikataa kuchukua hatua;
- Maelezo ya mbinu zote zilizotumiwa kutathmini mtoto wako, rekodi kuhusu mtoto wako na ripoti ambazo wilaya ilitumia kufanya uamuzi wake ili kuchukua hatua hiyo ama kutochukua hiyo hatua;
- Maelezo ya chaguzi zingine timu ya IEP iliangalia kwa ajili ya mtoto wako na sababu za kwa nini ilikataa chaguzi hizo; na
- Maelezo ya mambo mengine yaliyohusika katika uamuzi wa wilaya wa kuchukua ama kutochukua hatua.

Wilaya ya shule pia lazima ikupe habari kuhusu msaada wa kisheria wa bila malipo ama wa bei nafuu na huduma zingine zinazohusika ambazo ungeweza kupata.

Ikiwa lalamiko la mchakato wa kutatua mgogoro limeandikishwa dhidi yako wewe kama mzazi, lazima ujibu lalamiko hilo ndani ya siku 10 za kalenda. Jibu lako lazima lizungumzie waziwazi masuala yaliyotokea katika lalamiko la mchakato wa kutatua mgogoro.

### Utoshelevu

Lalamiko la hatua zinazotarajiwa huchukuliwa kama la kutosha (kumaanisha kwamba liliandikishwa ifaavyo) ***isipokuwa tu kama*** huyo mshiriki mwingine ajulishe ofisa msikilizaji asiyebagua na mshiriki aliye wasilisha lalamiko linalodai kwamba halijafikia matakwa ya kuandikisha (yaani, haitoshi). Mshiriki huyo mwingine lazima athibitishe utoshelevu wa lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro kwa maandishi, ndani ya siku 15 za kalenda wakati ambapo lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro lilipokewa.

Kwa mfano, ukiwasilisha lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro kwa wilaya yako (na upeleke nakala kwa Idara ya Elimu ya Ohio), itachukuliwa kama ya kutosha isipokuwa wilaya ikijulisha ofisa msikilizaji, kwa maandishi na ndani ya siku 15, kwamba haoni kama ombi lako limeandikishwa vifaavyo. Aidha, ofisa msikilizaji ako na siku tano za kalenda kuanzia anapopokea notisi yako ya wilaya iliyoandikwa ya kuamua ikiwa lalamiko lako la mchakato wa utatuzi wa mgogoro linatosha (ya kwamba linafikia mahitaji ya lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro yanayotambulishwa katika ukurasa wa 21). Ofisa msikilizaji lazima pia atume uamuzi wake kwako na kwa wilaya, kwa maandishi, ndani ya siku 15.

Ikiwa afisa msikizi ataamua kwamba lalamiko lako la mchakato wa utatuzi wa mgogoro halitoshi, una nafasi ya kuandikisha upya tena lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro ama kurekebisha lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro la mwanzoni, maadamu wilaya ikubali na iko na fursa ya kusuluhisha hali hiyo kupitia mkutano wa uamuzi ama ofisa msikilizaji apeane ruhusa kabla ya siku tano kabla mwanzo wa usikilizaji.

Ukirekebisha lalamiko lako la mchakato wa utatuzi wa mgogoro ifaavyo, basi kipindi cha siku 30 za uamuzi (ona ukurasa wa 23)huanza wakati ambapo unaandikisha lalamiko lililorekebishwa.

## Utatuzi wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro

### Kipindi cha Utatuzi

Kipindi cha uamuzi ni kipindi cha wakati kati ya kuandikisha lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro na usikilizaji halisi wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro. Kipindi cha utatuzi huhusisha mkutano wa utatuzi ambao huandaa fursa, kwa mara nyingine, kusuluhisha mgogoro wa elimu ya kipekee kabla usikilizaji kuanza rasmi. Ukiandikisha lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro lakini baadaye ukose kushiriki katika mchakato wa utatuzi, hii itachelewesha mwanzo wa mpangilio wa nyakati za mchakato wa utatuzi wa mgogoro (mengi zaidi kuhusu mpangilio wa nyakati yako hapo chini).

Kipindi cha utatuzi ni siku 30 kuanzia tarehe ambayo lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro liliandikishwa (ama kuanzia ile tarehe lalamiko lilirekebishwa ifaavyo). Ikiwa wilaya ya shule haijasuluhisha lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro hadi uridhike wakati ambapo siku 30 zimepita, usikilizaji wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro unaweza kuendelea. Mara tu kipindi cha siku 30 kimekamilika, kuna wakati wa siku 45 kwa ajili ya usikilizaji wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro na kwa ajili ya ofisa msikilizaji asiyebagua kufanya uamuzi (ona ukurasa wa 24), isipokuwa tu kama wewe na wilaya mmekubaliana upatanisho ambao unapita siku 30. Pia jua kwamba kipindi cha siku 30 kinaweza kamilika mapema iwapo, katika siku hizo 30, wewe na wilaya mmekubaliana katika maandishi kwamba maafikiano hayawezekani.

Katika kipindi cha siku 30 za utatuzi, na ndani ya siku 15 za kwanza za kalenda za kupokea lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro, shule ya wilaya lazima iratibu mkutano wa utatuzi. Ikiwa wilaya haitafanya mkutano wa utatuzi ndani ya siku 15 za kalenda ama haitashiriki katika mkutano wa utatuzi, huenda ukaomba afisa msikizi aanzishe mpangilio wa mchakato wa stahili. Wilaya haihitajiki kuratibu mkutano wa utatuzi ikiwa iliandikisha lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro.

### Mkutano wa Utatuzi

Madhumuni ya mkutano wa utatuzi ni kukupa fursa ya kujadili matatizo yaliyoko kwa lalamiko na wilaya ya shule ipate nafasi ya kushirikiana nawe katika utatuzi. Wajibu wa kuitisha mkutano wa utatuzi ni wa wilaya, na unahitajika kushiriki. Ikiwa hautashiriki katika mkutano wa utatuzi na wilaya iandike hati za kutoshiriki kwako, wilaya inaweza kumwomba ofisa msikilizaji kutupilia mbali lalamiko lako la mchakato wa utatuzi wa mgogoro mwishoni mwa kipindi cha siku 30.

Wewe na wilaya ya shule huamua kwamba ni wanachama gani wa timu ya IEP ambao wanafaa kuhudhuria mkutano wa utatuzi. Mkutano huu lazima ujumuishe mwakilishi wa wilaya ya shule ambaye ana mamlaka ya kufanya uamuzi kwa niaba ya wilaya.

Mwanasheria wa wilaya hatahudhuria mkutano huu isipokuwa ukitaka wakili wako ahudhurie. Mkutano huu ni hatua inayohitajika katika mchakato wa utatuzi isipokuwa kama wewe na wilaya mkubaliane kwa maandishi ama wewe na wilaya mkubaliane kutumia upatanisho badala ya mkutano wa utatuzi. Wewe na wilaya mmeruhusiwa kuleta mapatano kupita kipindi cha siku 30 za utatuzi ikiwa nyinyi wawili mmekubaliana hivyo. Hili litazuia kuanzia kwa usikilizaji wamchakato wa utatuzi wa mgogoro wa siku 45 na mpangilio wa uamuzi.

Ikiwa wewe na wilaya mtatatua mgogoro wenu katika mkutano wa utatuzi, lazima nyinyi wawili mtie saini katika makubaliano ya kubana kisheria ambayo:

- Yanaweka wazi kwa maandishi kitakachotokea;
- Yametiwa saini na wewe pamoja na mwakilishi wa wilaya; na
- Koti inaweza kuyatekeleza.

Makubaliano ya kisheria humaanisha kwamba ikiwa wewe ama wilaya ya shule haitashikilia makubaliano hayo, koti yaweza kukushurutisha wewe ama wilaya kufanya hivyo.

Ikiwa wewe wilaya ya shule mtaamua kutokubaliana, baada ya kutia saini kwenye makubaliano, mmoja wenu anaweza kufutilia mbali hayo makubaliano ndani ya siku za kazi baada ya kuitia saini.

Ikiwa wewe na wilaya ya shule mmekubaliana kuhusu lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro kabla kipindi cha siku 30 za utatuzi kimekamilika, lalamiko hilo litafungwa na usikilizaji wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro hautatendeka.

## Mchakato wa Usikilizaji

Usikilizaji wa hatua zinazotarajiwa lazima uratibiwe na uongozwe katika mahali fulani na kwa wakati ambao unakufaa wewe na wilaya ya shule. Ofisa msikilizaji asiyebagua atawasiliana nawe na wilaya wakati ule ule kila mara mawasiliano yanahitajika wakati wa mchakato wa usikilizaji. Yaani, mawasiliano yote kati ya ofisa msikilizaji asiyebagua, wewe na wilaya yatafanyika pamoja na sio kando kando.

Mpangilio wa usikilizaji wa siku 45 za mchakato wa utatuzi wa mgogoro (na kwa ajili ya ofisa mskilizaji asiyebagua afanye uamuzi) huanza baada ya kipindi cha siku 30 za utatuzi kukamilika ama baada ya mojawapo ya haya kutendeka:

- Wewe na wilaya mkubaliane kwa maandishi kutupilia mbali (kutokuwa na) mkutano wa utatuzi; ama
- Mara tu mtakapoanza kujadili masuala hayo katika mkutano wa utatuzi ama mkutano wa upatanisho, wewe na wilaya mkubali kwa maandishi kwamba maafikiano hayawezekani; ama
- Wewe na wilaya mkubali kwa maandishi kupitisha kipindi cha siku 30 za utatuzi ili muweze kuendelea kuleta mapatano, halafu wewe ama wilaya ijiondoe kwa mchakato wa upatanisho.

Isipokuwa kama ofisa msikilizaji asiyebagua akubali kuongeza muda (au kwa maneno mengine, ametoa idhini ya nyongeza), kufuatia ombi la mmoja wa washiriki ndani ya mpangilio wa siku 45 za usikilizaji, yafuatayo yatatendeka:

- Usikilizaji lazima ufanyike;
- Uamuzi wa usikilizaji lazima ufikiwe; na
- Lazima wewe, pamoja na wilaya ya shule, na vilevile Idara ya Elimu ya Ohio mtumiwe nakala ya uamuzi huo kupitia barua inayoidhinishwa.

Angalau siku tano kabla usikilizaji wa hatua zinazotarajiwa, wewe na wilaya ya shule lazima mshiriki katika mkutano wa kufunua. Haya ni mazungumzo ya kuhakikisha kwamba wewe pamoja na wilaya mko na habari ambayo itatolewa kwenye usikilizaji.



### Usikilizaji wa Mchakato wa Utatuzi wa Mgogoro Hufanywa na Ofisa Msikilizaji Asiyebagua

Wakati lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro haliwezi kutatuliwa, litaelekea kwa usikilizaji rasmi ambao utafanywa na ofisa msikilizaji asiyebagua. Ofisa msikilizaji lazima awe wakili aliyefunzwa kuongoza usikilizaji wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro na Idara ya Elimu ya Ohio.

Wilaya ya shule hulipia gharama za ofisa msikilizaji, hata hivyo yeye ni mtu asiyehusika moja kwa moja ambaye hapendelei upande wowote. Yeye hajaajiriwa na wilaya ya shule ama shirika lingine la elimu ya umma na huenda asiwe na maslahi ya kibinafsi ama ya kitaalamu ambayo ingependelea mshiriki mmoja juu ya yule mwingine.

Isitoshe, afisa msikilizaji anafahamu vizuri matakwa ya elimu ya kipekee, pamoja na IDEA, sheria na kanuni za serikali na jimbo na jinsi koti hufafanua kesi za elimu ya kipekee.

Baada ya usikilizaji, afisa msikilizaji ataandika uamuzi kulingana na utaratibu wa kisheria wa kawaida. Wilaya yako ama Idara ya Elimu ya Ohio inaweza kuandaa orodha ya maofisa wasikilizaji na sifa zao, ama unaweza kupata orodha hiyo kwa kutembelea education.ohio.gov, na utafute haya maneno makuu, *maofisa wa usikilizaji wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro.*

### Haki za Usikilizaji

Katika usikilizaji wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro, uko na haki ya:

- Kuandamana na mtoto wako ambaye ni mhusika wa usikilizaji;
- Kuomba kwamba usikilizaji ufunguliwe kwa umma;
- Kuwa na wakili ama watu wenye ujuzi wa pekee juu ya watoto walemavu wakuwe pamoja nawe na wakupe ushauri;

  Wasilisha uthibitisho (ushahidi), kukabili na kuhoji (dadisi) mashahidi na kushurutisha hudhurio la mashahidi (tena, usikilizaji utashughulikia tu masuala ambayo ulitaja katika lalamiko lako la mchakato stahili, isipokuwa wilaya ikubali utaje masuala mapya);
- Kukataza kuleta ushahidi wowote ambao haujaonyeshwa angalau siku tano za kazi kabla ya usikilizaji; na
- Bila gharama yoyote kwako, upokee rekodi ya usikilizaji ulioandikwa neno kwa neno, ama ukipenda wa kielektroniki, na rekodi zozote za matokeo na maamuzi

#### Ikiwa Unaandamana na Watetezi Ambao Sio Wanasheria

Ikiwa unaandamana na watetezi wowote ambao sio wanasheria, watu hawa hawastahili kupokea ada ya wakili (mwanasheria), (ama ada yoyote kwa ajili ya huduma zao) kutoka kwa mshiriki huyo mwingine. Mtetezi hawezi kufanya kazi ya uwakili katika usikilizaji na kuhusika kwa mtetezi huenda ukawa mdogo wakati wa shughuli hiyo.

### Kuharakisha Malalamiko ya Mchakato wa Utatuzi wa Mgogoro na Wakati

Kuharakishwa kwa usikilizaji wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro ni usikilizaji wenye mpangilio wa haraka ambao hurahisisha utatuzi wa migogoro fulani ya elimu. Wewe au wilaya inaweza kuwasilisha ombi la kuharakisha usikilizaji wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro katika hali hizi iwapo tu:

1. Hukubaliani na uamuzi wa wilaya ya shule kuhusu uwekaji wa kielimu wa mtoto wako (mpango ama huduma), na hii ndio sababu ya shule kuadhibu mtoto wako; ama
2. Hukubaliani na matokeo ya udhihirisho wa azimio; ama
3. Shule ya wilaya ina amini kwamba uwekaji wa hivi sasa wa kielimu wa mtoto wako (mpango ama huduma) una uwezo mkubwa wa kujeruhi mtoto wako ama watoto wengine.

Mpangilio wa lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro linaloharakishwa hujumuisha kipindi cha siku 15 za kalenda za utatuzi na mpangilio wa usikilizaji wa siku 20 za shule. Shule ya wilaya lazima iratibu mkutano wa utatuzi ndani ya siku saba za kalenda za kupokea lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro. Baada ya usikilizaji unaoharakishwa wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro kukamilika, ofisa msikilizaji ana siku 10 za shule za kuandika uamuzi wa mwisho na kuikimu kwako na wilaya. Hakuna muda wa ziada ambao utaongezwa katika wakati wa kuharakisha lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro.



## Kukata Rufaa

Uamuzi unaofanywa na ofisa msikilizaji asiyebagua katika hitimisho ya usikilizaji wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro ni wa mwisho isipokuwa kama mshiriki anayelalamika atawasilishe rufaa moja kwa moja hadi kwa Idara ya Elimu ya Ohio ndani ya siku 45 za kupokea uamuzi. Mshiriki anayedhulumiwa ni mzazi ama wilaya wakati ambapo uamuzi wa ofisa msikilizaji haufai kwa huyo mshiriki (ambalo humaanisha kwamba mshiriki huyo hakushinda).

### Jinsi ya Kukata Rufaa Uamuzi wa Ofisa Msikilizaji

Kukata rufaa ya uamuzi wa ofisa msikilizaji, lazima utume nakala ya rufaa yako katika maandishi kwa Idara na nakala ya rufaa kwa msimamizi wa wilaya ya shule yako. Idara itateua ofisa mkaguzi wa daraja ya jimbo (ofisa mkaguzi) kuongoza ukaguzi usiobagulika wa uamuzi wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro. Idara ya Elimu ya

Ohio italipa gharama za ofisa mkaguzi. Ofisa mkaguzi atachunguza rekodi za usikilizaji mzima wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro. Isitoshe, ofisa mkaguzi atahakikisha usikilizaji ulifuata mahitaji ya mchakato wa utatuzi wa mgogoro na atatafuta ushahidi wa ziada kama inavyohitajika. Ofisa mkaguzi anaweza kuomba majadiliano ya mdomo ama ya maandishi kutoka kwako na wilaya ya shule. Ikiwa ofisa mkaguzi ataongoza usikilizaji ili kutafakari majadiliano ya mdomo, haki zote za usikilizaji (angalia ukurasa wa 25) ambazo unapewa katika usikilizaji wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro vivyo hivyo utazipata wakati wa usikilizaji.

**Kuomba Rufaa ya Uamuzi wa Ofisa Msikilizaji Asiyebagua**

Unaweza kupinga uamuzi wa afisa msikilizaji asiyebagua (rufaa) kwa njia ya maandishi ndani ya siku 45 za kalenda za kupokea uamuzi huo. Tuma rufaa yako kwa:

Ofisi ya Idara ya Elimu ya Ohio ya
Watoto wa Kipekee,
Sehemu ya Utatuzi wa Migogoro
25 South Front Street
Mail Stop 409
Columbus, Ohio 43215

Kwa msaada zaidi, tafadhali pigia simu Ofisi ya Idara ya Elimu ya Ohio ya Watoto wa Kipekee kwa (614) 466-2650, ama simu isiyolipishwa kwa (877) 644-6338.

### Wakati/Ngogeza

Ndani ya siku 30 baada ya Idara kupokea ombi lako la ukaguzi wa daraja la jimbo, ofisa mkaguzi atatoa uamuzi, isipokuwa yeye atoe idhini ya nyongeza, ambayo inaweza kuombwa na mzazi ama wilaya (hata hivyo, jua kwamba nyongeza ya muda haiwezi kuruhusiwa wakati wa rufaa kutokana na usikilizaji wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro unaoharakishwa). Huenda pia ukaomba rekodi za ofisa mkaguzi za matokeo na uamuzi wa kielektroniki ama nakala zilizoandikwa ama rekodi za kielektroniki za neno kwa neno.

### Kukata Rufaa katika Mahakama ya Kitaifa ama ya Jimbo

Uamuzi wa ukaguzi wa daraja la jimbo ni wa mwisho isipokuwa ukatiwe rufaa kwenye mahakama ya kitaifa ama ya jimbo. Mshiriki anayedhulumiwa (hapati ushindi) na uamuzi wa ofisa mkaguzi ana haki ya kuwasilisha kesi katika mahakama ya wilaya ya taifa ndani ya siku 90 kuanzia tarehe ya uamuzi wa ofisa mkaguzi ama mahakama ya maombi ya kawaida ya kaunti ambayo shule ya wilaya ya mtoto wako inapatikana ndani ya siku 45 za kupokea notisi ya uamuzi wa ofisa mkaguzi. Mahakama itapitia rekodi, isikilize ushahidi zaidi kufuatia ombi la washiriki na ifanye uamuzi wa mwisho kulingana na rekodi na uthibitisho uliotolewa. Lazima ulipe gharama za mahakamani za rufaa unayowasilisha kotini, lakini ukishinda, huenda ukapewa haki ya kupokea ada za kotini na za wakili (angalia ukurasa wa 28) kwa hiari ya mahakama.

## Hali ya Mtoto Wakati wa Mchakato wa Utatuzi wa Mgogoro

- Mtoto wako lazima abaki ama aendelee kukaa katika uwekaji wa wakati huu ya kielimu wakati lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro unaedelea, isipokuwa kama wewe na wilaya ya shule mtakubaliana kwamba uwekaji wa kielimu wa mtoto wako unaweza kubadilishwa.
- Uwekaji wa kielimu wa mtoto wako wa wakati huu ndio umefafanuliwa katika IEP yake iliyotekelezwa hivi karibuni.
- Ikiwa mtoto wako amewekwa katika mpito mbadala wa mpangilio wa kielimu (IAES- ni mpangilio wa muda wa kujifunza nje ya shule) kwa sababu ya nidhamu kutokana na wilaya ya shule, mtoto wako hubaki katika mpangilio huo wa kielimu hadi ofisa msikilizaji afanye uamuzi ama hadi nidhamu ya wilaya kwa mtoto wako ikamilike, chochote kitakachotendeka cha kwanza.
- Ikiwa lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro linahusisha kuingia kwa wilaya, mtoto wako, kwa ruhusa yako, lazima awekwe katika wilaya hadi hatua zinazotarajiwa zikamilike.
- Ikiwa lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro linahusisha ombi la kuanzishwa kwa huduma za sehemu ya wenye chini ya umri wa kwenda shule kwa sababu mtoto wako amefika umri wa miaka 3 na hastahiki kupokea huduma chini ya sehemu ya sheria ya usaidizi wa mapema, wilaya ya shule haihitajiki kutoa huduma za usaidizi wa mapema ambazo mtoto wako hajakuwa akipokea.
- Ikiwa inapatikana kuwa mtoto wako anastahiki kupokea huduma za elimu ya kipekee na mzazi akubali uandalizi wa huduma mwanzoni, basi wilaya ya shule lazima itoe huduma hizo ambazo haziko katika mabishano kati ya mzazi na wilaya.
- Ikiwa ofisa mkaguzi anakubaliana na wazazi wa mtoto kwamba badiliko la uwekaji linafaa, uwekaji lazima uchukuliwe kama makubaliano kati ya jimbo na wazazi kwa madhumuni ya kuendelea kukaa.

## Ada za Wakili

Huenda ukamwajiri wakili (mwanasheria) wakati wowote akuwakilishe katika mchakato wa utatuzi wa mgogoro (ama shughuli za rufaa ya uamuzi wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro), lakini lazima ulipe gharama zako za kisheria. Ukichagua kumwajiri wakili na upate ushindi (upate uamuzi unaofaa) katika tendo lolote ama shughuli zinazohusiana na usikilizaji wako wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro (kukufanya uwe mshiriki anayeshinda), mahakama inaweza kuamrisha wilaya ikulipe kiasi kinachofaa cha ada za wakili.

### Ikiwa Wilaya Itashinda

Ikiwa wilaya itashinda, mahakama inaweza kukuamrisha ulipe kiasi kinachofaa cha ada za wakili wa wilaya. Mahakama inaweza kukuamrisha wewe ama wakili wako alipe ada ya wakili wa Idara ya Elimu ya Ohio ama wilaya a shule yako ikiwa watashinda na mahakama iamue yoyote yafuatayo:

- Kwamba tendo lilikuwa la upuuzi, lisilo na busara ama halina msingi;
- Kwamba uliendelea kuleta hatua za kisheria baada ya tendo hilo waziwazi likawa la upuuzi, lisilo na busara ama lisilo na msingi; ama
- Kwamba tendo lililetwa kwa sababu ya kusudi isiyofaa, kama vile kuhangaisha, kusababisha ucheleweshaji usio wa lazima, ama kuongeza bila sababu gharama ya ada ya kisheria.

### Mahakama Ikiamuru Ada za Kisheria zirejeshwe Kwako ama kwa Wilaya

Ikiwa mahakama itaamuru ada za kisheria zirejeshwe kwako ama kwa wilaya, mahakama itaamua kiasi kinachofaa. Ada za wakili ni lazima zitegemee kiwango cha ajira kilicho kawaida katika jamii ambayo tendo ama utaratibu lililetwa na aina ya ubora wa huduma zinazotolewa. Kuna mipaka fulani katika uwezo wa mahakama kuhukumu ada ya wakili. Mahakama haiwezi kuhukumu ada ya wakili katika mifano hii:

- Ambako wilaya inatoa ahadi ya kusuluhisha mgogoro kwa maandishi ndani ya siku 10 za utendaji, ukose kukubali hiyo ahadi kati ya siku 10, na uamuzi wa mahakama katika kesi hii uwe sio wa kufaa kwako kuliko maafikiano ambayo wilaya ilipendekeza kukupa;
  - Hata hivyo, mahakama inaweza kuamua upate ada ikiwa umeshinda hilo tendo na mahakama iamue kwamba unastahiki pa kubwa (ulikuwa na sababu nzuri ) ya kutokubali maafikiano ambayo wilaya ilipendekeza kukupa;
- Kushiriki kwa wakili wako katika mkutano wa IEP isipokuwa mkutano huo uliitishwa kwa sababu ya usikilizaji wa msimamizi ama hatua ya mahakama; na
- Kushiriki kwa wakili wako katika mkutano wa utatuzi.

### Kupunguza Ada za Wakili

Mahakama pia inaweza punguza uamuzi wa ada za wakili ikiwa:

- Wakati utaratibu unapoendelea, wewe ama wakili wako bila busara mlichelewesha suluhisho la mwisho kwa ajili ya mgogoro;
- Kiwango cha ada ya wakili kimepita juu kiasi kuliko kiwango cha ajira cha kila saa moja ambacho ndicho kimeenea katika jamii kwa huduma kama hizo kutoka kwa mawakili wenye ustadi unaopatana kiakili, sifa na uzoefu;
- Wakati uliotumiwa na huduma za kisheria ulizopokea zilipita kiasi (mingi mno) kutokana na hali ya tendo ama utaratibu;
- Wakili wako hakutoa habari inayofaa kwa wilaya ya shule katika notisi yako ya lalamiko.

Hakuna yoyote yaliyotajwa hapo juu yanayohusika ikiwa mahakama itapata kwamba jimbo au wilaya ya shule bila busara ilichelewesha utatuzi wa mwisho wa tendo ama utaratibu au vinginevyo ilikiuka hifadhi za mienendo ya IDEA.

# Nidhamu

## Taratibu za Kinidhamu kwa Watoto wenye Ulemavu

Kitika visa fulani, wilaya ya shule yako huenda ikalazimika kuendelea kutoa huduma za elimu ya kipekee kwa mtoto wako aliye na ulemavu, hata baada ya wilaya imesimamisha, kufukuza au vinginevyo kumtoa mtoto wako kutoka kwa uwekaji wa kielimu wa wakati huu (rejelea IEP ya mtoto wako kwa habari zaidi kuhusu uwekaji wake wa kielimu wa wakati huu).

### Uwekaji wa Kielimu na Chaguo Nyingine

Ikiwa mtoto wako ameondolewa kutoka kwa uwekaji wa kielimu wa wakati huu kwa ajili ya kukiuka sheria za wilaya ya shule kwa chini ya siku 10 mfululizo za shule, wilaya hailazimiki kumpatia mtoto wako huduma za elimu ya kipekee katika wakati huo. Ikiwa mtoto wako ameondolewa shuleni***kwa zaidi ya siku 10 mfululizo za shule***, shule lazima iendelee kupatia mtoto wako huduma za elimu ya kipekee, hata kama ni katika mazingira mengine tofauti (kwa mfano, darasa lingine, jengo, ama nyumbani kwa mwanafunzi).

Ikiwa shule ya wilaya imeondoa mtoto wako kutoka kwa maangusho yake ya wakati huu kwa zaidi ya siku 10 mfululizo katika mwaka huohuo wa shule, inaonwa kuwa badiliko la maangusho ya elimu ya mtoto wako.

Ikiwa wilaya ya shule imeondoa mtoto wako kutoka kwa uwekaji wa kielimu wa wakati huu katika vipindi tofauti-tofauti (mfululizo wa kuondolewa) ambazo hujumlika zaidi ya siku 10 katika mwaka wa shule, wilaya lazima ibainishe kama huko kuondolewa hufanyiza badiliko la uwekaji wa kielimu wa mtoto wako. Katika kufanya azimio hii, wilaya inapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:

- Urefu wa kila muda ambao mtoto wako aliondolewa;
- Jumla ya wakati ambao mtoto wako aliondolewa;
- Jinsi huko kuondolewa kunakaribiana pamoja; na
- Mfanano wa tabia za mtoto wako kwa tabia zake katika matukio ya hapo awali ambapo mtoto wako aliondolewa.

Wakati wa kubadilisha uwekaji wa kielimu wa mtoto wako kwa sababu mtoto wako hakufuata sheria za shule, wilaya ya shule, mzazi na wanachama wanaofaa wa timu ya IEP lazima wakutane kukagua kudhihirisha azimio. Madhumuni ya ukaguzi wa kudhihirisha azimio ni kubainisha kama tabia ya mtoto wako ilisababishwa ama ilikuwa na uhusiano wa moja kwa moja na ulemavu wa mtoto wako.



## Kudhihirisha Azimio

Kabla ya kubadilisha uwekaji wa kielimu wa mtoto wako kwa sababu za kinidhamu, wilaya ya shule inapaswa kuchukua hatua fulani kulinda haki za mtoto wako. Hatua moja ni kufanya mkutano wa ukaguzi wa kudhihirisha azimio. Huu ni mkutano wa kubainisha kama tabia ya mtoto wako ilisababishwa au ilikuwa na uhusiano wa moja kwa moja na ulemavu wa mtoto wako. Kwa maneno mengine, je tabia ya mtoto wako ilisababishwa na ulemavu wake? Timu ya IEP ya mwanafunzi itaamua kama tabia ya mtoto wako ilisababishwa na ulemavu ndani ya siku 10 za shule za uamuzi wowote wa kubadilisha uwekaji wa kielimu.

**Tafadhali Jua kwamba**

**Mtoto wako anapaswa kutii sheria na nidhamu kama watoto wale wengine shuleni na ataendelea kupokea huduma zinazoelezwa katika IEP, lakini huenda asiwe katika uwekaji sawa.**

### Mkutano wa Ukaguzi wa Kudhihirisha Azimio

Katika mkutano wa ukaguzi wa kudhihirisha azimio, wewe na wanachama wengine wa timu ya IEP hupitia habari muhimu pamoja na IEP ya mtoto wako, uchunguzi wa mwalimu na habari yoyote husika iliyotolewa.

Ikiwa hiyo tabia ni dhihirisho la ulemavu wa mtoto wako, mtoto wako atarejeshwa kwa uwekaji ambao yeye aliondolewa, isipokuwa timu ya IEP ikikubali badiliko la uwekaji.

Ikiwa tabia ya mtoto wako inapatikana kuwa ni dhihirisho la ulemavu, timu ya IEP inapaswa:

1. Kuanza tathmini inayoathiri tabia ndani ya siku 10 na kuimalizia haraka iwezekanavyo. Tathmini inayoathiri tabia ni ukaguzi wa tabia ya mtoto wako ambao hutumika kubainisha kile, katika mazingira ya mtoto wako, husababisha tabia isiyofaa, na vile vile ni tabia gani mbadala zinahitaji kufundishwa ndio mtoto wako apate matokeo na majibu mazuri; na
2. Kuanza mpango wa kurekebisha tabia kwa ajili ya mtoto wako ikiwa tathmini inayoathiri tabia tayari imekamilika na inahusiana na nidhamu iliyopo. (Mpango wa kurekebisha tabia hushughulikia tabia ambazo hazifai shuleni na njia mahsusi ambazo shule itajaribu kuzipunguza.); ama
3. Ikiwa mpango wa kurekebisha tabia tayari upo, pitia huo mpango na ufanye mabadiliko yoyote yanayohitajika ndani ya siku 10.



## Mpango Mbadala (Wa muda na Tofauti) wa Kushiriki Kielimu

Uamuzi wa kuweka mtoto wako katika mpango mbadala wa kushiriki kielimu (IAES) hufanywa na timu ya IEP ya mtoto wako. IAES ni uwekaji tofauti wa muda kwa ajili ya mtoto wako kupokea elimu ya kipekee. Ile siku timu ya IEP itafanya uamuzi wa kubadilisha uwekaji wa mtoto wako hadi kwa IAES kwa sababu mtoto wako amekiuka sheria za shule, wilaya ya shule lazima ikujulishe kuhusu uamuzi huo na ikupe huu Mwongozo wa Haki za Wazazi katika Elimu ya Kipekee.

Hata kama tabia za mtoto wako zilisababishwa na ulemavu wake, wilaya huenda ikaondoa mtoto wako kwa IAES kufikia siku 45 za shule ikiwa mtoto:

- Alibeba silaha;
- Kwa kujua alimiliki ama kutumia mihadarati, ama akauza ama akajaribu kununua kitu ambacho kimedhibitiwa (kwa mfano, dawa za kulevya); ama
- Alisababisha kwa mtu mwingine majeraha makubwa ya mwili.

Hii kwa ujumla hutumika ikiwa mtoto wako alitenda kinyume cha tabia alipokuwa akienda shuleni, akiwa shuleni ama katika adhimisho la shule.

Ikiwa tabia ya mtoto wako ***haikusababishwi moja kwa moja na ulemavu*** wake, mtoto wake anaweza kuwekwa kwa IAES kwa kiwango kilekile cha wakati ambacho mtoto asiye na ulemavu angetiwa nidhamu.

Ikiwa tabia ya mtoto wako ***ilihusiana moja kwa moja ama ilisababishwa na ulemavu*** wake na mtoto wako akakiuka sheria za shule, mtoto wako lazima arudishwe kwa mpangilio wa elimu ambao yeye alitolewa, isipokuwa wewe na wilaya ya shule mkubaliane badiliko la uwekaji kama sehemu ya mabadiliko katika mpango wa kurekebisha tabia ama IEP.

Hata hivyo, ikiwa wilaya inaamini kwamba kuweka mtoto wako katika uwekaji wa kielimu wa wakati huu (kulingana na IEP ya mwanao) inaelekea sana kusababisha jeraha kwa mtoto wako ama wengineo, shule ya wilaya huenda ikaitisha mkutano wa IEP ili kujadili jambo hili. Ikiwa wewe ama wilaya mkose kukubaliana kuhusu badiliko la uwekaji, wilaya huenda ikaomba usikilizaji ulioharakishwa wa hatua zinazotarajiwa - yaani, huenda ikaomba usikilizaji wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro ambao utaharakishwa kwa ajili ya utatuzi wa haraka (Angaia hatua kuharakishwa kwa mchakato wa utatuzi wa mgogoro katika ukurasa wa 25).

### Ikiwa Hutakubaliana na Badiliko la Uwekaji wa Kielimu ama Matokeo ya Usikilizaji ya Ukaguzi wa Kudhihirisha Azimio

Unaweza kuomba usikilizaji ulioharakishwa wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro ili kupinga uamuzi wa kubadilisha mpangilio wa elimu ya mtoto wako wa wakati huu kwa sababu ya nidhamu ama kupinga matokeo ya ukaguzi wa kudhihirisha azimio. (Angalia habari kuhusu mchakato wa utatuzi  wa mgogoro katika ukurasa wa 24 - 25). Ofisa msikilizaji asiyebagua atatoa uamuzi wakati wa usikilizaji ulioharakishwa wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro kama wilay aya shule ilifuata matakwa ilipobadilisha uwekaji wa mtoto wako ama ikiwa wilaya imeonyesha kwamba tabia ya mtoto wako ilikuwa ama haikuwa dhihirisho la ulemavu wa mtoto wako..


Kama ilivyotajwa hapo juu, wilaya ya shule huenda ikaomba usikilizaji ulioharakishwa wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro ikiwa wilaya inaamini kwamba kuendeleza uwekaji wa mtoto wako kunaelekea sana kusababisha jeraha kwa mtoto wako ama wengineo. (Ona kuharakishwa kwa mchakato wa utatuzi wa mgogoro katika ukurasa wa 25).

### Wakati Ambapo Tabia ya Mtoto Wako Hutokana na Tuhuma ya Ulemavu

**Ikiwa mtoto wako hana IEP, unaweza kuomba shule ichukulie mtoto wako kama mtoto mwenye ulemavu ikiwa yoyote haya yalitendeka kabla mtoto wako kukiuka sheria za shule:**

- **Uliambia viongozi wa shule ama mwalimu wa mtoto wako, kwa maandishi, kwamba unafikiri mtoto wako huenda akahitaji huduma za elimu ya kipekee; ama**
- **Uliomba tathmini ya mtoto wako; ama**
- **Mwalimu wa mtoto wako ama mfanyakazi mwingine wa wilaya ya shule aliambia mkurugenzi wa elimu ya kipekee wa wilaya ama wasimamizi wengine moja kwa moja juu ya mambo mahsusi yanayohusu mpangilio wa tabia ya mtoto wako.**

**Wilaya ya shule yako haipaswi kutarajiwa kuchukulia mtoto wako kama mwenye ulemavu ikiwa umekataa kupatia wilaya ya kutathmini mtoto wako kwa ajili ya elimu ya kipekee. Hilo ni kweli pia ikiwa ulikataa elimu ya kipekee na huduma husika kwa ajili ya mtoto wako ama ikiwa mtoto wako alitathminiwa na timu ikaamua kwamba mtoto wako hana ulemavu. Wilaya inaweza kuadhibu mtoto wako kwa njia sawa kama vile ingewaadhibu wanafunzi wasio na ulemavu ambao mienendo yao ni hiyo hiyo.**



# Uwekaji wa Upande mmoja na Wazazi kwa ajili ya Watoto wenye Ulemavu katika Shule za Binafsi kwa Gharama ya Umma

## Mchakato wa Kubaini Kurejesha Gharama

Ukiamua kupeleka mtoto wako katika shule ya kibinafsi, wilaya yako hailazimiki kulipa gharama ya elimu au ya elimu ya kipekee na huduma husika katika hiyo shule ya kibinafsi mradi tu wilaya imetoa kwa mtoto wako elimu inayofaa ya umma bila malipo (FAPE) katika wilaya. Ikiwa unaamini kwamba wilaya yako ilishindwa kutoa kwa mtoto wako FAPE, una fursa ya kuandikisha lalamiko la mchakato wa utatuzi wa mgogoro ambamo usikilizaji utaongozwa na ofisa msikilizaji asiyebagua atatoa uamuzi ili kuona kama wilaya ilitoa FAPE kwa mtoto wako (Angalia habari kuhusu hatua zinazotarajiwa  katika ukurasa wa 21-27). Ikiwa itaonekana na ofisa msikilizaji asiyebagua wakati wa hatua zinazotarajiwa kwamba wilaya haikutoa FAPE, ofisa msikilizaji anaweza kuamua kwamba uko na haki ya kurejeshewa (kurudishiwa pesa) pesa unazogharamia kuandikisha mtoto wako katika shule ya kibinafsi.

### Kupunguka ama Kutwaliwa kwa Marejesho ya Gharama

Kiwango cha pesa ambacho wilaya inapaswa kurudisha kwako huenda ikapunguzwa ama unaweza kupoteza marejesho ya gharama kabisa ikiwa yoyote yafuatayo yatatendeka:

- Katika mkutano wa IEP ambao ulifanyika kabla umetoa mtoto wako kwa shule, hukuambia shule ya kwamba haukuwa ukubali uwekaji wa kielimu uliopendekezwa na timu ya IEP na uwaambie kuhusu mahangaiko yako, na kwamba ulipanga kuandikisha mtoto wako katika shule ya kibinafsi; ama
- Hukuambia shule kwa maandishi angalau siku 10 za kazi kabla ya kumtoa mtoto kutoka kwa wilaya kwamba hutakubali IEP na unapanga kuandikisha mtoto wako katika shule ya kibinafsi. Hizi siku 10 za kazi hujumuisha sikukuu zilizopo katikati ya juma; ama
- Iwapo kabla ya kutoa mtoto wako kutoka shule, wilaya ilikupa notisi iliyoandikwa ifaavyo kusema kwamba ilipanga kutathmini mtoto wako, na hukuhakikisha mtoto wako anapatikana kwa sababu ya tathmini; ama
- Mahakama iamue kwamba ulitenda bila kutumia busara.

### Ulinzi wa Marejesho ya Gharama

Marejesho ya gharama (kiasi utakachorudishiwa) haiwezi kupunguzwa, ama malipo hayawezi kukataliwa kwako ikiwa:

- Wilaya ilikuzuia kutoa notisi;
- Wilaya haikukujulisha kwamba ulihitajika kutoa notisi; ama
- Kutoa notisi kungeweza kutokeza dhara la kimwili kwa mtoto wako.

Pia, mahakama ama ofisa msikilizaji anaweza kugundua kwamba marejesho ya gharama hayawezi kupunguzwa ama kukataliwa kwako kwa kushindwa kutoa notisi hii ikiwa:

- Huwezi kusoma ama kuandika kwa Kiingereza; au
- Kutoa notisi kungeweza kutokeza madhara makubwa ya kihisia kwa mtoto wako.



# Taarifa kwa Mzazi kuhusu Programu za Msaada wa Masomo kwa Wanafunzi wenye Ulemavu

## Wakati Taarifa Inatolewa

Kila wakati shule ya wilaya hukamilisha tathmini ya mtoto aliye na ulemavu, au ikianza kutayarisha, kukagua ama kurekebisha IEP ya mtoto, wilaya lazima ijulishe mzazi wa mtoto kuhusu Mpango wa Kulipia Wanafunzi wenye Ugonjwa wa akili Masomo na Mpango wa Kulipia Masomo wa Jon Peterson.

### Mpango wa Kulipia Wanafunzi wenye Ugonjwa wa akili Masomo

Ikiwa mtoto wako anapokea huduma za elimu ya kipekee chini ya kikundi cha ugonjwa wa akili wa watoto, huenda ukastahili kupata Mpango wa Kulipia Wanafunzi wenye Ugonjwa wa akili Masomo. Chini ya mpango, huenda ukaamua kumtuma mtoto wako kwa mpango wa elimu ya kipekee ambao ni tofauti na ile inaendeshwa na wilaya yako ya shule unapoishi, ambapo mtoto wako atapokea elimu na huduma inayoelezwa katika IEP yake.

Ili mtoto wako astahiki kuwa ndani ya mpango lazima awe:

- Amegunduliwa na wilaya ya shule yako unapoishi kwamba ni mtoto mwenye ugonjwa wa akili wa watoto;
- Lazima awe na IEP ya wakati huu kutoka kwa wilaya ya shule unapoishi ambayo unakubaliana nayo na imekamilishwa; na
- Lazima angalau awe na umri wa miaka mitatu.

Kwa habari kuhusu Mpango wa Kulipia Wanafunzi Wenye Ugonjwa wa Akili Masomo, tembelea tovuti ya Idara ya Elimu ya Ohio kwa education.ohio.gov na uandike maneno ***Mpango wa Kulipia Wanafunzi Wenye Ugonjwa wa Akili Masomo***katika kisanduku cha utafutaji, au utume barua pepe kwa **autismscholarship@education.ohio.gov**.

### Mpango wa Kulipia Wanafunzi wenye Mahitaji ya Kipekee Masomo wa Jon Peterson

Ikiwa mtoto wako anapokea huduma za elimu ya kipekee, huenda ukastahili kupata Mpango wa Kulipia Wanafunzi wenye Mahitaji ya Kipekee Masomo wa Jon Peterson.  Chini ya mpango, huenda ukaamua kumtuma mtoto wako kwa mpango wa elimu ya kipekee ingine tofauti na ile inaendeshwa na wilaya ya shule yako unapoishi, ambapo mtoto wako atapokea elimu na huduma inayoelezwa katika IEP yake.

Kustahili kupata Mpango wa Kulipia Wanafunzi wenye Mahitaji ya Kipekee Masomo wa Jon Peterson, mtoto wako:

- Lazima awe amegunduliwa na wilaya ya shule ya eneo lako kuwa yeye ni mtoto mwenye ulemavu;
- Lazima awe na IEP ya wakati huu kutoka kwa wilaya ya shule unapoishi ambayo unakubaliana nayo na imekamilishwa; na
- Lazima astahili kuhudhuria shule ya chekechea hadi darasa la 12.

Kwa habari kuhusu Mpango wa Kulipia Wanafunzi wenye Mahitaji ya Kipekee Masomo, tembelea tovuti ya Idara ya Elimu ya Ohio kwa education.ohio.gov na uandike maneno ***Jon Peterson Scholarship*** kwenye kisanduku cha kutafuta, au barua pepe **peterson.scholarship@education.ohio.gov**.

### Taarifa za Ziada

taarifa kuhusu mipango ya kulipia masomo inapatikana katika tovuti ya Idara ya Elimu ya Ohio kwa **education.ohio.gov**.

Kwa taarifa zaidi au maswali kuhusu mipango hii ya kulipia masomo, wasiliana na:
Ofisi ya Nonpublic Educational Options kwa (614) 466-5743 au simu isiyolipishwa kwa: (877) 644-6338.

Ohio | Department of Education

education.ohio.gov